# Nipashe

Jumamosi Oktoba 12, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580047

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

w...ter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Ndugu feki waibuka, wasababisha uhamishaji makaburi kusitishwa

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM aamuru JWTZ kudhibiti ujambazi

• **Ni** kutokana na kukithiri uhalifu Katavi, atangaza msako mkali wa silaha, awaambia wakimbizi... *Endelea ukurasa 2*



Nyumba zikiwa zimezingirwa na mafuriko ya maji katika eneo la Mto Amtico kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Mji wa Muheza mkoani Tanga, jana. **Picha ndogo;** wananchi wakiangalia daraja la reli inayotoka Tanga kwenda bara kupita kwenye mto huo, likiwa limebomoka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Mdaiwa wizi benki abambwa 'gesti'

UKURASA 3



## Kikwete ageuka mbogo wapotoshaji kauli zake

• **Awataka** wawe jasiri na kujitokeza badala ya kujificha 'nyuma ya pazia'... *Uk. 2*

**MICHEZO** YANGA YAKUTANA KUIJADILI PYRAMIDS UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri Jafo awachongea Ma-RC kwa Rais Magufuli

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, amemwomba Rais John Magufuli, kupokea dokezo lake la mapendekezo ya kuwachukulia hatua viongozi wa mikoa na wilaya ambao watafanya vibaya kwenye uandikishaji wapigakura uchaguzi wa serikali za mitaa.

Pia amesema uandikishaji wa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi huo si wa kuridhisha kwa mikoa yote nchini na kwamba kinachokosekana ni uhamasishaji.

Jafo aliyasema hayo jana mbele ya Rais wakati wa mkutano wa hadhara baada ufunguzi wa barabara ya Mpanda – Uvinza mkoani Katavi, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kiongozi huyo.

Kwa mujibu wa Jaffo, mikoa iliyofanya vizuri kuwa ni pamoja na Iringa ambao imefikisha asilimia 53 ukifuatiwa na Mbeya, Songwe na Tanga.

Alisema katika tathmini hiyo, Mkoa wa Dar es Salaam una asilimia nane huku Kilimanjaro ikiwa na asilimia 12 na Arusha asilimia 13.

"Naomba uridhie uandikishaji unaisha Ocktoba 14, mwaka huu. Haiwezekani siku ya mpira wa Simba na Yanga watu wote wanaenda uwanjani lakini siku ya uandikishaji watu wanasuasu. Endapo siku saba zitakwisha na kuna mikoa haijafika hata asilimia 50 nitaomba nilete dokezo kwako," alisema.

"Kuna wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, kuna wakurugenzi itakapobainika watu walizembea katika kuhamasisha watu kujiandikisha, nitaomba wachukuliwe hatua," alisema.

Alisema agenda ya uchaguzi wa serikali za mitaa ndiyo inayotoa mchakato wa maendeleo na kwamba ikibainika kuwa watu wengi walizembea kuhamasisha watu kujiandikisha, atapeleka pendekezo maalum kwa Rais Magufuli kwa hatua zaidi.



Rais Dk. John Magufuli akiangalia ramani ya majengo ya hospitali ya Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi jana, wakati akipewa maelezo na Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo (kushoto), katika eneo la mradi huo wa ujenzi. Wa (tatu kushoto), ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA: IKULU**

# JPM aamuru JWTZ kudhibiti ujambazi

**Na Beatrice Moses**

RAIS John Magufuli ameuweka Mkoa wa Katavi chini ya uangalizi wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), kutokana na kukithiri kwa vitendo vya uhalifu na ujambazi, vinavyohusishwa na wakimbizi.

Amesema kuna baadhi ya wakimbizi ambao wameficha silaha kwenye vichaka hivyo serikali inafuatilia kwa karibu ili kuwanasa wakaonyeshe walikowauzia.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana akiwa katika Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi, wakati akizindua kipande cha barabara ya Mpanda - Uvinza iliyojejwa kwa kiwango cha lami.

Aliagiza JWTZ kupitia Brigedi ya 201 ya Tabora kutekeleza jambo hilo huku akisisitiza kuwa nchi haiwezi kuchezewa na mtu yeyote. "Kwa hiyo Jeshi la Wananchi Tanzania mpeleke base pale. Brigedi ya 201 ya Tabora ndiyo watakuwa wanahudumia hapa kwa sababu ni karibu. Nchi hii haiwezi kuchezewa na mtu yeyote. Kama kuna mkimbizi anafikiri anaweza kuichezea amepotea, tunahitaji upendo wa kweli mambo ya kui-beep Tanzania hayapo.

"Wapo walioishi miaka mingi, wapo waliopewa uraia na wapo wachache wameanza kuharibu sifa za ukimbizi kwa kujihusisha na ujambazi," alisema

Aidha, aliongeza kuwa kumekuwa na matukio ya uhalifu wa maliasili katika msitu wa Tongwe na kwamba baadhi ya wakimbizi wanaoaminika kuwa na silaha wamekuwa wakihusishwa.

"Waache tabia hiyo mara moja wamekimbia kule kutokana na migogoro waliyoisababisha wao. Ukija hapa kaa utulie, hapa si mahali pa kuleta migogoro na ukikimbilia taifa lingine kaa utulie usijifanye unajua," alisema.

Pia alisema serikali haina matatizo na wakimbizi ambao ni watulivu kwa kuwa nchi inawapokea kwa maslahi mapana lakini wanapowashambulia wakulima wakiwa shambani, kuvamia mabasi na kupora abiria serikali kazima iingilie kati.

Rais Magufuli aliwataka wakimbizi waliopokewa watulie kwenye maeneo waliyopangiwa kuishi na wasitumie nafasi zao kuwapeleka wenzao huko.

Alisema mauaji ambayo

INAENDELEA UK.8

# JK awa mbogo wapotoshaji kauli zake

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, ametaka watu wenye maoni yao wawe jasiri kuyasema na waache tabia ya kujificha katika kivuli cha hotuba yake aliyoitoa hivi karibuni katika kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Katibu wa Ofisi ya Kikwete ikiwa ni siku nne tangu kongamano hilo lifanyike, hotuba ya Kikwete katika kumbukizi hizo za miaka 20 haikulenga kuwasema baadhi ya viongozi waliopo sasa.

"Wapo wanaojaribu kuweka maneno kinywani mwake (Kikwete) ambayo hakuyasema husisani waliodai alikuwa akiwasema baadhi ya viongozi waliopo sasa," taarifa hiyo ilisema.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa mada katika kongamano hilo ambalo liliandaliwa na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere, ilikuwa urithi wa Mwalimu Nyerere katika uongozi, maadili, umoja na amani katika ujenzi wa taifa.

"Katika hotuba yake alimwelezea (Nyerere) alivyomfahamu. Kilichotushangaza na kutusikitisha sisi na Rais Mstaafu ni kujitokeza watu wanaopotosha ukweli kuhusu maneno aliyosema.

"Kamwe hakumzungumzia mtu mwingine yeyote zaidi ya Mwalimu Nyerere. Hakufanya ulinganifu wa kati ya Nyerere na marais walifuata baada yake, waliostaafu na waliopo sasa. "Katika hotuba yake hakumtaja mtu yeyote. Tunaposikia wakidai Rais (mstaafu) alikuwa anamsema mtu, ni jambo linalotusikitisha na kutusononesha. Ni uzandiki, fitina na uchonganishi," ilisema taarifa hiyo.

Rais mstaafu, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alitazamia sana watu wamkosoe kwa yale aliyoyasema kuhusu Mwalimu Nyerere na si kuzungumzia mambo ambayo hakuyasema.

"Amewataka watu wenye maoni yao wawe jasiri kuyasema na waache tabia ya kujificha katika kivuli cha hotuba yake," ilisema. Akifungua kongamano hilo Jumanne ya wiki hii, Kikwete alitaja mambo kama tisa ambayo Mwalimu Nyerere enzi za utawala wake aliyasimamia.

Jambo la kwanza, alisema Nyerere ndiye mkombozi kutoka katika mikono ya wakoloni na la pili, ni ni karama alizopewa kwa kuendesha harakati za kudai uhuru kwa maneno na kupatikana kwa maneno bila kumwaga damu.

Jambo la tatu, ni imani ya haki na umoja wa Afrika na Afrika Mashariki na kwa kushirikiana na Abeid Amani Karume, walianzisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni urithi mkubwa.

Kikwete, alisema jambo la nne, Nyerere alijenga taifa lenye umoja, amani na mshikamano miongoni mwa raia huku akibainisha jambo la tano kuwa aliheshimu utu wa mtu pamoja na ukubwa wote aliokuwa nao kama Rais alikuwa wa kawaida mbele ya wengine.

Kwa mujibu wa Kikwete, jambo la sita, Mwalimu aliamini uhuru wa Tanganyika hauna maana kama bado hata nchi moja ya Afrika itakuwa bado imetawaliwa ndiyo maana alihakikisha kudai uhuru wa nchi mbalimbali.

"Jambo la saba, Mwalimu Nyerere aliwapenda vijana na alitambua umuhimu wa kuwalea na alikuwa karibu na Umoja wa Vijana na kutoa fursa kwao ya kuanza kujifunza uongozi, kujifunza kusema, kutoa mawazo na kujifunza kutambua jinsi nchi inavyoendeshwa.

Jambo la nane, Kikwete alilitaja kuwa ni Mwalimu Nyerere aliamini katika meza ya mazungumzo na kutolea mfano mwaka 1988, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) walifanya maandamano kupinga wabunge kujiongezea mishahara.

Alisema katika kikao cha Kamati Kuu walilijadili jambo hilo na baada ya kupitia makaratasi ya waandamanaji, walitoa msimamo wa wakasema huo ni uhaini wakamatwe waweke ndani lakini Nyerere aliwaeleza kuwa mawazo hayapigwi rungu, mawazo yanashindwa na mawazo yaliyo bora zaidi.

Jambo la tisa alisema Nyerere alikuwa hatishwi na hoja na kwamba hoja haipigwi rungu bali inashindwa na hoja iliyo bora zaidi ya ile iliyotolewa.

# Ndugu feki wakwamisha uhamishaji wa makaburi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amesitisha uhamishaji makaburi katika eneo la Chinyoya yaliyotakiwa kuondolewa kupisha ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), baada ya kubaini kuna mamluki wa ndugu wa marehemu.

Katambi alisitisha kazi hiyo jana baada ya kupokea malalamiko ya baadhi ya ndugu wa marehemu waliozikwa katika eneo hilo kabla ya kuanza kuhamisha mabaki hayo hadi baada ya kikao cha pamoja alichoagiza kifanyike jana mchana.

"Ninajua kuna watu wametoka mbali kuja hapa kwa ajili ya jambo hili lakini nawaomba kusitisha kwanza ili baada ya kikao, tutalifanya kesho (leo) asubuhi na mimi nitakuwepo kulisimamia," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema alipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya ndugu na familia za watu waliozikwa hapo kwamba hawakuwapo wakati wa kuhakiki ndugu wa watu waliozikwa eneo hilo, hivyo walipofika wakashangazwa kuambiwa kuwa makaburi yote ndugu walishapatikana.

"Sitaki kuwaumiza watu mara mbili. Walipofiwa waliumia kwa kuondokewa na mpendwa wao na leo tena tuwaumize kwa kuwapa ndugu bandia kaburi? Haiwezekani, serikali yetu ni sikivu, hivyo tuvumiliane ili haki itendeke," alisema.

Mmoja wa ndugu waliozikwa eneo hilo, Mary Ndahani, aliishukuru serikali kwa kuingilia kati jambo hilo ili kila familia inayohusika na watu waliozikwa hapo watendewe haki.

INAENDELEA UK.8

# Mvua zasababisha madhara makubwa

**Na Steven William** MUHEZA

MVUA zimeleta madhara maeneo mbalimbali nchini, huku katika wilaya za Korogwe na Muheza, watu tisa wamefariki dunia kwa kuangukiwa na nyumba walimokuwa wamelala na wengine kusombwa na maji.

Aidha, mvua hizo zimesababisha uharibifu wa miundombinu ikiwamo reli kusombwa eneo la Korogwe, hivyo kufanya treni za mizigo kushindwa kupita.

Tuta la eneo la reli lilizolewa na maji na kuacha shimo kubwa ambalo limesababisha huduma za usafiri wa reli hiyo kusitishwa kwa muda.

Viongozi wa serikali mkoani Tanga wamethibitisha kutokea kwa madhara hayo na kwamba hatua mbalimbali zimechukuliwa huku wananchi wakitakiwa kuchukua tahadhari.

Katika maafa hayo, kaya 150 hazina makazi na shehena ya mizigo iliyokuwa inakwenda Bandari ya Tanga, baada ya kipande cha reli kuzolewa eneo la Muheza imekwama.

Wilayani Muheza, watu wanne wameokolewa kufa maji baada ya kuzingirwa na maji katika Mto Mkurumuzi wakati wakijaribu kuvuka kwenda ng'ambo.

Aidha, mji wa Muheza ulizidi kuingiliwa na mafuriko

INAENDELEA UK.8



Kamanda wa polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Gilles Muroto, akionyesha kwa waandishi wa habari jijini humo jana, fedha taslimu Sh. milioni 37, zilizokamatwa na jeshi hilo, zinazodaiwa kuibwa katika Benki ya Exim, tawi la Dodoma, Agosti 29 mwaka huu. Fedha hizo ni kati ya zaidi ya Sh. milioni 140 zilizoibiwa katika benki hiyo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mtuhumiwa wa wizi benki abambwa gesti na mil. 37/-

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MTUNZA fedha wa benki ya Exim tawi la Dodoma, Martine Temu (33), anayedaiwa kuiba Sh. milioni 141.9, amedakwa na jeshi la polisi akiwa amejificha kwenye nyumba ya kulala wageni mkoani Singida.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema jana kuwa wizi huo ulitokea Agosti 29, mwaka huu na mtuhumiwa alitokomea kusikojulikana baada ya tukio hilo.

"Aliiba fedha za Kitanzania milioni 120, USD 9,513 (Sh. milioni 21.8) na Euro 50 (Sh. 125,890). Baada ya kufanya wizi alitoroka kwenda mafichoni. Msako mkali ulifanyika na kufanikiwa kumkamata mkoani Singida akiwa amejificha kwenye nyumba ya wageni iitwayo Manonga," alisema.

Muroto alisema mtuhumiwa huyo alikutwa akiwa na Sh. milioni 37.5 kati ya fedha anazodaiwa kuiba.

"Yupo mshiriki mwingine jina tunalihifadhi na msako mkali dhidi yake unaendelea. Mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani wakati wowote,"alisema.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limemkamata Isack Okwango (27) mkazi wa Buzuruga, Mwanza na Buguruni jijini Dar es Salaam katika nyumba ya kulala wageni ya Erickson Lodge iliyoko Makole jijini hapa akiwa na jeki moja, bisibisi na simu tatu za wizi, kamera, komputa mpakato moja aina ya Toshiba na kisu.

Kamanda alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Oktoba 6, mwaka huu, akiwa katika nyumba hiyo na amekuwa akitafutwa kwa muda mrefu kwa tuhuma za kuvunja nyumba usiku na amekuwa akihama mikoa kwa ajili ya kufanya uhalifu.

Wakati huo huo, Mkazi wa Nyakato, Ashraf Sani (31) amekamatwa kwa tuhuma za wizi wa magari yaliyoegeshwa kwa muda katika sehemu za kumbi za starehe kwenye sherehe na mikutano.

Muroto alisema mtuhumiwa huyo alikuwa amepanga chumba katika nyumba ya kulala wageni Sweetland iliyoko Bahi Road jijini hapa.

Alisema mtuhumiwa huyo amekamatwa akiwa na rimu tisa, matairi matano, jeki mbili na spana. Kamanda huyo alisema mbinu anazotumia ni kutumia gari lake lenye namba za usajili T 793 CFT Nissan kulisogeza karibu na gari analotaka kuiba na kuweka jeki na kufungua matairi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

11/10/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 13/10/2019 kampuni ya CHINA SICHUAN INTERNATIONAL COOPERATION (SIETCO) itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka SONGEA kuelekea IRINGA Gari yenye namba za usajili T 586 DMF / T 369 DNW

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19 |
| Upana | - | mita | 2.95 |
| Kimo | - | mita | 4.5 |

3. Njia itakayotumika: SONGEA hadi IRINGA kupitia NJOMBE
Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115458802



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**05-10-2019**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 13-10-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Chang'ombe, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 636 DFA / T 887 DJB**
**T212 BTE/T 574 BZB**
**T653 DFA/T 900 BAZ**
**T195 BTE/T837 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **27** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.1** |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam Port hadi Chang'ombe kupitia Mandela road, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215454002

# Ukatili wa kijinsia wazidi kushika kasi

Na Romana Mallya

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia nchini katika kipindi cha miaka miwili kilichoanzia mwaka 2017, yameongezeka kutoka 41,416 hadi 43,487.

Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi Tanzania, Mary Nzuki, alitoa taarifa hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa jengo litakalotumika kama dawati la jinsia katika Kituo cha Polisi Kawe. Jengo hilo ambalo limejengwa pembeni mwa kituo hicho, ni msaada kutoka mradi wa Save the Children kwa kushirikiana na ubalozi wa Sweden ambao pia wamekabidhi pikipiki moja ambayo itasaidia polisi kufuatilia matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye jamii.

Nzuki alisema katika kipindi cha mwaka 2017, matukio ya ukatili wa kijinsia ambayo yalipokelewa kwenye madawati mbalimbali vituo vya polisi yalikuwa ni 41,416.

Alisema mwaka jana matukio yaliyoripotiwa kwenye madawati hayo yalikuwa 43,487 sawa na ongezeko la matukio 2,071.

"Mkoa wa Kinondoni matukio yaliyoripotiwa kwa kipindi cha mwaka 2017 yalikuwa 7854 na mwaka 2018 yalipungua na kufikia 5,386. Katika kukabiliana na changamoto hizi kwenye jamii, Jeshi la Polisi limetoa mafunzo kwa askari 7,000 na tuna jumla ya madawati 450 kama haya nchi nzima. Tunawashukuru Save the Children kwa msaada huu mliotupatia," alisema. Nzuki alisema kabla ya ujenzi wa jengo hilo, kituo cha Kawe kilikuwa kinatumia kontena lililopo hapo kama ofisi ya dawati lakini sasa kimepata ofisi ambayo imejengewa ukuta itakayowafanya wanaofika kutoogopa kutoa taarifa zao.

"Mazingira ya jengo yanamruhusu mtu kueleza shida zake bila woga na anakuwa huru. Lakini bado tuna changamoto kwa wanaotoa taarifa za ukatili wa jinsia. Kesi nyingi zimekuwa zikiishia kufutwa mahakamani kwa sababu mashahidi wamekuwa hawajitokezi," alisema.

Kwa mujibu wa Nzuki, mara nyingi matukio hayo yanaporipotiwa na familia kwa sababu baadhi huhusisha ndugu na inapofikia hatua ya kutaka ushahidi, wamekuwa hawajitokezi na mwisho kumkosesha haki yule aliyetendewa kitendo hicho. Nzuki alitaja aina mbalimbali za ukatili kuwa ni ule wa kimwili, kisaikolojia, wa kiuchumi na wa kingono.

Katibu Tawala Wilaya ya Kinondoni, Stella Msofe, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alipongeza Save the Children ambayo imekuwa ikishirikiana na serikali katika maeneo mbalimbali. Aidha, aliitaka jamii kutowalea wanaofanya matukio ya ukatili wa kijinsia kwa sababu ni wahalifu kama majambazi na majangili.

"Kuwaacha bila kuwachukulia hatua kwanza unamfanya yule aliyefanyiwa tukio kama ni mtoto baadaye apate msongo wa mawazo, wito wangu kwa jamii endeleeni kuyaibua matukio haya ili wahusika wachukuliwe hatua," alisema. Mkurugenzi kutoka Save the Children, Dar es Salaam, Angela Makota, alisema wamekabidhi jengo hilo jana ikiwa ni siku ya mtoto wa kike wa Afrika.

"Mradi wetu unataka wale wanaokuja vituoni kupata huduma baada ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia wapate ulinzi, wasijisikie aibu kuzungumza na watoe ushirikiano kwa polisi ili wahusika wakamatwe," alisema.

Alisema ripoti ya mwisho ya mwaka 2015 inaeleza kwamba theluthi tatu ya watoto wote wa kike na wakiume, wasichana ni asilimia 72 na wavulana ni 71 ambao wamepitia katika hatua za manyanyaso. Mwaka 2018, alisema mradi huo umewafikia watu 466,167 na katika hao 245,499 ni afua za ulinzi wa mtoto.

Pia alisema walifikia watu 9,622 katika afua ya haki za watoto na utawala, 12,289 katika afua za elimu, 10667 katika dharura, 200,667 kupitia miradi ya afya na lishe.

# Kabendera aomba msamaha wa Rais

Na Elizabeth Zaya

WAKILI Jebra Kambole anayemtetea Mwandishi wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, ameijulisha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa mteja wake anataka kujadiliana na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) namna ya kumaliza kesi inayomkabili.

Wakili Kambole alisema hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile wa Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu, Dar es Salaam.

Alisema Kabendera anafanya mchakato huo wa kujadiliana na DPP kwa mujibu wa kifungu namba 194 A(2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Kesi ya Kabendera ilifika mahakamani hapo jana kwa ajili ya kutajwa huku upande wa Jamhuri ukieleza kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Wakili wa Serikali Wankyo Simon, alikiri kuhusu taarifa za Kabendera kupanga kufanya majadiliano na DPP.

Simon alidai kuwa taarifa hiyo ni ya kweli na wako katika mchakato na kusisitiza kwamba taratibu zikikamilika wataijulisha mahakama.

Taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari na Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, ilithibitisha kuwa jopo la mawakili wameelekezwa na Kabendera kuhusu kusudio hilo.

"Jopo la mawakili chini ya maelekezo ya Kabendera likiongozwa na Kambole, limeijulisha mahakama kwamba kwa mujibu wa kifungu namba 194 A (2)

INAENDELEA UK.8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitazama nyanya wakati alipozindua mradi wa mafunzo ya kilimo kupitia tekinolojia ya kitalu nyumba kwenye viwanja vya Nanenane, Ngongo, Lindi juzi. **PICHA: OWM**

# Muhimbili yatoa uvimbe bila upasuaji

Na Mary Geofrey

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imeanza kutibu uvimbe kwenye kizazi bila kufanya upasuaji kwa kuingiza mpira wenye chembechembe maalum kwenye mishipa ya damu ambazo zinakwenda kuziba mishipa inayopeleka damu kwenye uvimbe.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Radiolojia ya MNH, Dk. Frola Lwakatare, alisema baada ya mishipa kuziba, uvimbe unakosa damu au chakula chake na hivyo kusinyaa na kufa.

Dk. Lwakatare alisema mwanamke mwenye uvimbe kwenye kizazi endapo atapatiwa tiba hiyo, hakuna haja ya kumfanyia upasuaji mkubwa wa kuondoa uvimbe tena.

"Bila kufanya upasuaji kama inavyofanyika kwa wagonjwa wengi, tunaendelea sasa kutibu uvimbe kwenye kizazi (uterine fibroids) bila kufanya upasuaji. Hadi sasa wagonjwa wanne wamepatiwa huduma hii kupitia tiba radiolojia," alisema Dk. Lwakatare.

Aidha, alisema wameendelea kutoa huduma za utoaji wa sampuli kutoka kwenye uvimbe sehemu mbalimbali za mwili ambazo si rahisi kufikiwa bila upasuaji mkubwa, kuzibua mirija ya nyongo, kuweka mirija kwenye figo ambayo mirija ya mkojo imeziba na unyonyaji wa uvimbe wenye maji na usaha ikiwa ni mwendelezo wa huduma hiyo.

Dk. Lwakatare alisema MNH ilianzisha huduma ya kibingwa ya tiba radiolojia Novemba, 2017 iliyohusisha vifaa vya radiolojia kama X-Ray, Fluoroscopy, CT-Scan na Ultrasound kutibu moja kwa moja ugonjwa au kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi.

"Tumeendelea kutoa huduma ya uwekaji wa mipira maalum kwenye mshipa mkubwa wa damu (permanent catheter insertions) ambayo inanufaisha wagonjwa wa figo walio kwenye mfumo wa kusafisha damu (renal dialysis) au wanaopatiwa tiba ya saratani.

"Hii inaondoa usumbufu wa kutumia mishipa midogo ya mikononi ambayo mara nyingi ni ngumu kupatikana hasa kama inatumika mara kwa mara kwa muda mrefu," alisema Dk. Lwakatare.

**FAIDA YAKE**

Dk. Lwakatare alisema tiba hiyo inafaida kubwa kwa kuwa inawezesha tiba kwa kuepuka upasuaji mkubwa ambao una vihatarishi, kuepuka ukaaji wa hospitali kwa muda mrefu kwa sababu wanaofanyiwa tiba radiolojia mara nyingi huweza kurudi nyumbani siku hiyo hiyo, hivyo kupunguza gharama.

Alisema tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo, wagonjwa 558 wamepatiwa huduma ya kibingwa ya tiba radiolojia, huku 274 wakiwa wenye uvimbe wa kinywa na wengine 284 ni wa magonjwa mengine.

Kwa mujibu wa Dk. Lwakatare, hospitali imekuwa ikitoa huduma hiyo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Yale na vyuo vishiriki vya Marekani na ilianzisha programu maalum ya mafunzo ya tiba radiolojia

Alisema wakufunzi wamekuwa wanakuja nchini kwa awamu kuanzia Octoba mwaka 2018. Pia alisema wakufunzi walio nao ni kundi la 11 tangu ushirikiano huo uanze na imehusisha wakufunzi ambao ni daktari bingwa radiolojia, fundi sanifu radiolojia, muuguzi radiolojia kutoka Canada wakiongozwa na Dk. Ash Murray wa Toronto.

Alisema wiki chache zilizopita timu kama hiyo ilitoa mafunzo na huduma za tiba radiojia wakitokea Chuo kikuu Cha Emory kilichopo mji wa Atlanta nchini Marekani.

Timu ya tiba radiolojia, alisema imetoa mafunzo kwa wataalamu wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ili kuwawezesha kuweka mipira maalamu kwenye mishipa kama ilivyoelezewa kwa lengo la kuwawezesha wagonjwa wa Saratani kupata nafuu.

Alisema pia kuendelea kujengewa uwezo kwa watalaam wa ndani utasaidia kwa kiwango kikubwa kukuza huduma hiyo nchini na watalaam kutoka hospitalini na wanapata fursa ya kujifunza Muhimbili kwa gharama nafuu hivyo kuongeza idadi ya watoa huduma.



Magari yakilikwepa shimo lililopo kwenye barabara jirani na soko la Shekilango, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# MCT yaboresha tuzo uandishi wa habari

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limezindua rasmi Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania mwaka 2019, huku likiondoa baadhi ya makundi na kuingiza mapya.

MCT kupitia Kamati ya Maandalizi ya Tuzo za Umahiri, ilisema jana kuwa imeongeza makundi mapya matatu ya uandishi wa habari za ubunifu na maendeleo ya watu na uandishi wa habari za hedhi salama na afya ya uzazi.

Makundi yaliyoondolewa ni habari za usalama na ubora wa chakula, kodi na mapato, na habari za afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mukajanga, alisema ikiwa ni mara ya 11 kufanyika kwa tuzo hizo, tayari zimezaa matunda.

'Lengo kubwa la kuanzisha mashindano haya lilikuwa kuhamasisha waandishi wa habari kufanya kazi kwa bidii na ufanisi zaidi, kuhakikisha wanafanya kazi zinazoleta matokeo chanya na kuacha alama. Tumeshuhudia hayo yanafanyika na ndiyo mafanikio tuliyokuwa tunayataka na ni furaha kubwa kwetu," alisema Mukajanga.

Katika awamu ya 11 ya mashindano hayo, alisema habari zitakazoshindaniwa ni kutoka makundi 20 zikiwamo tuzo ya uandishi wa habari za uchumi, biashara na fedha; uandishi wa habari za michezo na utamaduni; uandishi wa habari za biashara na kilimo; uandishi wa habari za elimu; uandishi wa habari za utalii na uhifadhi na uandishi wa habari za uchunguzi.

Kajubi ambaye ni Katibu Mtendaji wa MCT, Makundi aliyataja makundi mengine kuwa ni uandishi wa habari za takwimu; uandishi habari za haki za binadamu na utawala bora; mpiga picha bora magazeti.

INAENDELEA UK.8

# Waziri ataka mageuzi uzalishaji asali

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ( TFS) kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo katika uzalishaji asali.

Kanyasu alisema hayo jana alipokuwa akizungumza mkoani Tabora na watumishi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii wakiwamo wa Chuo cha Nyuki Tabora

Alisema uzalishaji wa asali nchini hauridhishi hasa katika mikoa minane ya kimkakati ambayo wizara iliamua kuanza nayo. Mikoa hiyo ni Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Geita, Kigoma, Mbeya na Katavi.

Naibu Waziri alisema wizara inategemea kuona mikoa hiyo inatambuliwa kwa uzalishaji wa asali lakini suala hilo limechukua muda mrefu bila kuwa na utekelezaji wowote.

Kanyasu alisema masoko ya asali yamepatikana China na Marekani lakini imeshindikana kutokana na asali inayozalishwa nchini kuwa kidogo ambayo imekuwa ikikidhi mahitaji ya ndani pekee wakati kuna misitu mingi inayoweza kuzalisha asali nyingi kukidhi masoko yote.

Alisema ufugaji wa nyuki umekuwa ukipata msukumo mkubwa katika ngazi ya wizara lakini katika ngazi za chini

INAENDELEA UK.8

# Majaliwa ataja mbinu mbadala ya ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali imeamua kupambana na ukosefu wa ajira kwa vijana kwa kuanzisha programu za kuongeza na kurasimisha ujuzi.

Majaliwa alisema hayo juzi wakati akizindua mradi wa kitaifa wa mafunzo ya ujenzi na kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (greenhouse) kwenye viwanja vya maonyesho vya Ngongo, Lindi ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa kwa mwaka 2019.

"Mwelekeo wa serikali hivi sasa ni kuendeleza viwanda na viwanda hivi vinahitaji malighafi kutokana na mazao. Tumeamua kuongeza malighafi kupitia kilimo kwa lengo la kuwafanya vijana kuajiriwa kwenye sekta hii kubwa ya uzalishaji," alisema.

"Nataka vijana mwondokane na dhana ya kwamba kuwa na ajira ni lazima uwe umekaa mezani na umeshika kalamu. Ajira ni kazi yoyote halali inayompatia mtu kipato, iwe ni biashara ndogo ndogo, mamalishe au bodaboda," alisisitiza.

Kuhusu teknolojia ya kitalunyumba, Waziri Mkuu alisema: "Programu hii inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Serikali inayoongozwa na Rais John Magufuli imeweka msisitizo kwenye kilimo lakini tunaangalia na aina ya kilimo tulicho nacho.

"Maeneo mengi nchini hayana mvua za kutosha kwa hiyo tumeanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone na si kwa kuchimba mifereji. Kitalunyumba kinahitaji nafasi chini ya robo eka na humo ndani kuna matuta manne tu. Kwa kutumia tangi la maji, unatumia maji kidogo sana kwa kila mche kwa sababu yanatoka kwa matone."

Alisema mtu yeyote mwenye eneo la kutosha anaweza kutumia teknolojia ya kitalunyumba wakiwamo wafanyakazi ili wapate mazao ya kujiongezea mapato.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga maandalizi kuivaa Pyramids yaanze mapema

**BAADA** ya droo ya mechi ya hatua ya mtoano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika tangu Jumatano iliyopita, na Yanga kupangwa na Pyramids ya Misri, inamaanisha kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo yanatakiwa yaanze sasa.

Yanga ambao ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wataanza kwa kuwakaribisha Waarabu hao hapa nyumbani Oktoba 27 mwaka huu, na mchezo wa marudiano utachezwa Novemba 2 mwaka huu huko nchini Misri.

Ili kuhakikisha kuwa Yanga inafanya vema na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo, inahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya kwanza huku ikijiandaa kwenda kukamilisha ratiba huko ugenini.

Waswahili wanasema siku hazigandi, huu ndio muda muafaka wa Yanga kuanza maandalizi ya mechi hizo mbili za kimataifa, ambazo kama Yanga watafanikiwa kushinda, watakuwa wametinga hatua ya makundi ambayo itawaletea sifa kama klabu, vile vile itawapatia fedha.

Mbali na kuipa sifa klabu, tayari Yanga watakuwa wameipeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka kama walivyofanya watani zao, Simba kwenye msimu uliopita, ambao walifika hatua ya robo fainali.

Tunapenda kuwakumbusha viongozi, benchi la ufundi, wachezaji na wadau wote wa Yanga, huu ndio wakati wa kushikamana na kushirikiana kuhakikisha timu yenu inasonga mbele katika michuano hiyo na kuendelea kuipa Tanzania Bara pointi ambazo zitafanya iendelee kuwakilishwa na klabu nne katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Tunaamini kuwa timu iliyofanya maandalizi mazuri, ina nafasi kubwa ya kupata matokeo chanya na huu ndio wakati sahihi wa Yanga kujipanga kuwasoma wapinzani wenu ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuwafunga.

Nipashe linawakumbusha Yanga kuwa, kwenye dunia ya sasa, hakuna timu ndogo au kubwa, timu zote zilizofika hatua ya mtoano, zina hadhi na viwango vinavyofanana. Ila mshindi wa jumla katika mechi hizo mbili mtakazocheza, ndio atakuwa bora.

Ni vema wahusika wote muhimu, mkaanza mapema maandalizi ya kuhakikisha mnafanya vema katika dakika hizo 180 zinazowasubiri, lakini mkifanya vizuri zaidi katika dakika 90 za kwanza hapa nyumbani. Ushindi wa nyumbani, utawafanya wachezaji kuwa na morali na ari ya juu ya kwenda kumalizia kazi waliyoianza huko ugenini na si kujiweka katika "mlima mrefu" au kusema wanakwenda "kupindua meza" kama ilivyozoeleka.

Huku ikitumia mechi zake za ligi dhidi ya Alliance na Mbao FC itakazocheza (kama ratiba ya Ligi Kuu Bara iliyopo) kabla ya kuikaribisha Pyramids, haitabadilika kujiandaa kuwavaa Waarabu hao, ni vema pia ikawa na programu nyingine maalumu ya kuhakikisha wachezaji wake wanaandaliwa kushinda mchezo huo wa kimataifa.

Kuelekea mchezo wa kwanza dhidi ya Pyramids, Yanga inatakiwa iingie uwanjani ikiwaheshimu wapinzani wao na vile vile ikiufananisha mchezo sawa na fainali, hivyo inatakiwa kupata ushindi mnono ambao utawaweka kwenye nafasi salama na nzuri ya kusonga mbele.

Kama Simba iliweza kuwavua ubingwa vigogo Zamalek, Yanga pia inaweza kuwaondoa Pyramids ambayo ina miaka 11 tangu ilipoanzishwa na kamwe isitishwe na majina au nchi wanazotoka wachezaji walioko kwenye kikosi hicho ambacho kiko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Misri.

Hakuna kisichowezekana, endapo Yanga itafanya maandalizi mazuri na mapema, itasonga mbele katika michuano hiyo na kuwapa furaha mashabiki wake ambao waliumia baada ya kuona wametolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Zesco ya Zambia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Yanga bado haijakaa sawa!

Na Barnabas Maro

**"SIHADAIKE** na rangi, tamu ya chai ni sukari." Maana yake usidanganyike na rangi ya chai, utamu wake ni sukari.

Methali hii hutumiwa kumzindua mtu asipumbazike au asivutwe na sifa za kitu ila akichunguze kwa undani hakika ya kitu au jambo. Ndio makala yangu ya leo.

"Kusifiwa si kuona, shani (jambo au kitu cha kushangaza) ni kujionea mwenyewe." Hata ukasifiwa jambo na mtu aliyeshuhudia, haiwi sawa na kujionea mwenyewe. Heri kushuhudia jambo mwenyewe badala ya kuelezwa na aliyeshuhudia.

Kabla ya kuendelea, najitambulisha kwanza nilivyo. Nilijiunga na Yanga Desemba 2, 1966 na kukabidhiwa kadi namba 447 yenye picha ya mkono ulioshikilia mwenge. Mashabiki waliuita 'mkono wa Kilambo' (Mungu amrehemu) aliyekuwa beki machachari wa Yanga ya wakati ule.

Kadi zilipobadilishwa na kulipa malimbikizo ya ada za mwaka 1976 nilipewa kadi mpya mwaka 1977 yenye namba 01868 iliyoandikwa:

Daima mbele nyuma mwiko. Madhumuni ya Yanga: 1) Kudumisha na Kustawisha Michezo ya aina zote Tanzania. 2) Kushirikiana na Vyama vyote vya michezo katika Afrika na Ulimwenguni kwa Jumla.

Je, michezo ya aina zote imedumishwa na kustawishwa kwa mujibu wa kanuni ya kwanza? Je, ushirikiano wa Yanga na vyama vyote vya michezo katika Afrika na ulimwenguni kwa jumla umetendeka? Mbona siuoni au umri wangu (81 na miezi miwili) unanipiga teke?

Ahadi ya Mwana-Yanga: 3. Nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa chama na kushirikiana na wanachama wenzangu kukiimarisha Chama. Rushwa na Fitina ni adui wa chama changu nitasema kweli daima.

Wahenga walisema: "Kweli ndio fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Twakumbushwa umuhimu wa kuusema ukweli hata kama kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Tuseme kweli: Sisi ni waaminifu na watiifu kwa Yanga na tunashirikiana na wanachama wenzetu kukiimarisha chama chetu? (Sio chama letu iandikwavyo na magazeti ya michezo!)

Mbona baadhi yetu wamekuwa 'wanachama' wa kuinyonya Yanga na kujinufaisha kwa fedha zinazopatikana? Tunashirikiana? Mbona hakuna la maana tulilofanya hata Yanga kwenda arijojo (uendeshaji usio na mwelekeo mwafaka kwa kukosa kuongozwa au kupangiliwa vizuri)?

Mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao: (a) kuwa wakati wote mkweli na mwaminifu wa Klabu; (b) Kuwa wakati wote hadaiwi ada zozote za uanachama na (c) Kuhudhuria mikutano ya Klabu inayomhusu.

"Kweli ingawa chungu niambie sinifiche." Maana yake niambie kweli hata kama mchungu. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na tabia ya kusema kweli.

Sasa nazungumzia mechi ya Ligi Kuu baina ya Yanga na Coastal Union iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita.

Niliitazama mechi ile kwa makini mwanzo mpaka mwisho, lakini sikuwa na amani. Kilichonifanya nisiwe na amani ni namna wachezaji wa Yanga walivyosumbuliwa na wenzao wa Coastal Union kutoka Tanga.

Yanga waliondoka uwanjani na alama tatu dhidi ya Coastal Union kwa 'ushindi' wa bao 1-0. Ingawa timu yangu ndio 'iliyoshinda,' lazima niwe mkweli. Sikushangilia 'ushindi' tuliopewa na refa akisaidiana na mshika kibendera wake. Kwa nini? Sikuona vizuri msukumano uliotokea kwenye lango la Coastal Union!

Kama twataka kujenga timu yetu, twapaswa kujisahihisha na kujihukumu wenyewe bila soni kwani hakuna binadamu asiyekosea. Ili kujikosoa lazima tukubali tunapokosa.

Baadhi ya wanachama wenzangu na mashabiki watanichukia kwa kusema hayo lakini nasimamia neno hili: "Kweli ndiyo fimbo ya kukamata."

Ingawa ni kweli kuwa Yanga ndio timu iliyotwaa Kombe la Ligi Kuu ya Tanzania Bara mara nyingi kuliko timu zote zilizoshiriki na zinazoshiriki, ni kweli pia kuwa Yanga ya sasa yanipa shaka kama itafika mbali msimu huu!

Waandishi wa michezo walisifu sana usajili uliofanywa na Yanga msimu huu. Walisahau kuwa "mgema akisifiwa, tembo hulia maji."

Methali hii huweza kutumiwa kuwanasihi watu wasimsifu mtu sana asije akafura kichwa na kuharibika. Pia hutumiwa kwa mtu ambaye asifiwapo huishia kujivuna. Yangu macho.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 344 096**



Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kutoka Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, Dk. Eusebius Mbonde (kulia), akikabidhi msaada wa vifaa vya kufundishia vyenye thamani ya Sh. milioni 165, kwa Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kasulu, Ramadhani Simba, uliotolewa na Karibu Tanzania Organization (KTO), kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mtuhumiwa wa ubakaji bintiye akamatwa baada ya kuachiwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KIGOGO wa Taasisi Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropikali (TPRI), Aresteric Silayo, jana alikamatwa na polisi baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kutupilia mbali mwenendo wa shauri la ubakaji lililokuwa linamkabili.

Shauri hilo sasa limeamuriwa kusikilizwa upya mbele ya hakimu mwingine ili haki itendeke pande zote mbili kutokana na hakimu mkazi aliyekuwa anasikiliza kesi hiyo kudaiwa kukiuka baadhi ya vifungu vya sheria.

Hakimu Aziza Temu alitoa uamuzi huo jana mbele ya mahakama hiyo baada ya kupewa mamlaka na mahakama Kuu Kanda ya Arusha kusikiliza rufaa namba 101 mwaka ya mwaka huu kutokana na shauri namba 339/2017 ambalo hukumu yake ilitolewa Disemba 14 mwaka jana na Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Gwantwa Mwankuga

Akitoa uamuzi huo, Temu alisema mahakama hiyo imepitia mwenendo mzima wa shauri hilo na kubaini kuwa hakimu wa mahakama ya awali alikosea baadhi ya vifungu vya sheria ikiwamo sheria ya ushahidi iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2006.

"Sheria hiyo inamtaka hakimu kumwongoza mtoto kusema ukweli. Lakini hakimu alipuuzia sheria hiyo ambayo inaeleza mtoto mdogo anaweza kutoa ushahidi bila kiapo lakini aahidi kusema ukweli," alisema.

"Licha ya kumwongoza mtoto kusema ukweli, hakimu huyo alimhoji mtoto maswali mengi wakati sheria inaelekeza mtoto anatakiwa kuhojiwa maswali kidogo kisha kumwongoza katika kutoa ushahidi," aliongeza Hakimu Temu.

Hakimu pia alisema licha ya upungufu, ushahidi uliotolewa na upande wa Jamuhuri, akiwemo mwalimu wa darasa wa mtoto anayedaiwa kufanyiwa kitendo hicho, daktari na mwathirika mwenyewe, ulionyesha kwamba mtuhumiwa ametajwa mara nyingi kwamba alikuwa anamwingilia mwanawe hoja ambazo zilikuwa zinatosha kumtia mtuhumiwa hatiani.

Hakimu alisema kutokana na sababu hizo kimsingi usikilizwaji wa mwenendo mzima wa kesi hiyo ulikosewa hivyo ni vyema shauri hilo likasikilizwa upya na kwa haraka mbele ya hakimu mwingine Kuhusu upande wa wajibu rufani uliokuwa unaongozwa na Wakili John Materu, Hakimu Temu alisema shauri hilo lilikuwa la kutengeneza na kwamba limesheleweshwa mahakamani kwa nyakati licha ya Jamhuri kufuta shauri hilo.

"Kwa sababu hizi, ili haki itendeke pande zote mbili, ninaamuru shauri hili lirudi katika mahakama ya awali iliyokuwa inasikiliza kesi hiyo mbele ya hakimu mwingine na uendeshaji wake ufanyike mara moja kwa kuwa shauri limechukua muda mrefu," alisema.

Baada ya maelezo hayo, askari waliovaa sare na askari kanzu walimweka chini ya ulinzi kigogo huyo kisha kumpeleka kituo kikuu cha polisi cha Mkoa wa Arusha akiwa kwenye gari lenye namba za usajili T259 DPY.

# Watishia kumwona JPM kisa kijiji chao kufutwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAFUGAJI Jamii ya Kimasai katika kijiji cha Mabwegere, Kilosa mkoani Morogoro, wamesema wanakusudia kwenda kumwona Rais John Magufuli ili kuingilia kati juu ya kufutwa kwa kijiji chao.

Tangazo la kufutwa kwa kijiji hicho kubaki kuwa kitongoji kikiwa chini ya kijiji cha jirani cha Mfulu, lilieleza kuwa utaratibu na uanzishwaji wake haukufuatwa.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mika Kashu, aliwaeleza wananchi hao juzi alivyoliona tangazo lililobandikwa katika Ofisi yake na kukuta kijiji hicho hakipo katika orodha ya uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kashu alisema alipata tangazo la serikali kuwa kijiji hicho kimekuwa kitongoji katika kijiji cha Mfulu na kwamba katika uchaguzi wa kuwapata viongozi wa serikali za mitaa na kijiji, wanapaswa kupiga kura katika kijiji cha Mfulu.

Alisema kijiji hicho kilishafanya uchaguzi mara tano kuanzia awamu ya pili ya Rais Benjamini Mkapa hadi uchaguzi mkuu uliopita kabla ya kufutwa juzi na kuwa kitongoji.

"Kijiji chetu kwenye orodha kimewekwa kama kitongoji na si kijiji na hatujui sababu mpaka sasa. Nachukua nafasi hii kuwaarifu kuwa hatuna kijiji sasa hivi tutakuwa sehemu ya kijiji cha Mfulu,"alisema Kashu

Mwenyekiti mstaafu wa Mabwegere, Tondakai Mwasole, alishushwa na uamuzi uliofanywa na serikali ya wilaya ya Kilosa kwa kuwa kijiji hicho kilianzishwa kwa kufuata taratibu zote ikiwamo kuwa na uongozi unaotambulika akiwamo ofisa mtendaji wa kijiji pamoja na ofisi.

Alisema kutokana na kijiji hicho kufutwa, wanakusudia kwenda kumwona Rais Magufuli ili aingilie kati suala hilo na kwamba kwa sasa hawako tayari kushiriki uchaguzi wakiwa chini ya kijiji cha Mfulu.

" Sisi tulikuwa na kijiji chetu cha wafugaji cha Mabwegere na wakulima wana kijiji chao cha Mfulu. Leo tunaunganishwa kijiji kimoja na sisi kubaki kama kitongoji. Hatuko tayari, tutaenda kumwona Rais ili aingilie kati," alisema.

Naye Martha Moringe, alisema uamuzi wa kukifuta kijiji hicho ni uonevu uliofanywa na viongozi wa serikali kwa kuwa walikuwa na mgogoro na sisi kubaki kama mgogoro na vijiji vingine kwa ajili ya kuonyeshana mipaka na si mgogoro mwingine kama inavyoelezwa.



# Binti atoweka nyumbani kwao

**Na Elizabeth Zaya**

ASHURA Mzambele (27) mkazi wa Mbezi Kimara, Jijini Dar es Salaam, amepotea.

Mzazi wa binti huyo, Zuhura Feruzi, alisema jana kuwa mwanawe aliondoka nyumbani tangu Septemba 27, mwaka huu jioni na hajaonekana tena.

"Wakati anaondoka nyumbani alikuwa na mdogo wake na alijua kwamba anatoka tu mara moja halafu atarudi, lakini haikuwa hivyo," alisema Zuhura na kuongeza kuwa:

"Kibaya zaidi aliondoka na mtoto wake mdogo wa miezi sita tu ambaye alikuwa amembeba mgongoni, kwa hiyo wamepotea yeye na mtoto."

Mzazi huyo alisema mwanase alikuwa anasumbuliwa na tatizo la akili kwa vipindi.

"Mwanangu huwa ana tatizo kidogo la akili hususani unapoelekea mwisho mwa mwezi, kwa hiyo tunahisi tayari hilo tatizo litakuwa lilimkumba," alisema na kuongeza kuwa wamefanya jitihada za kumtafuta kwa ndugu na jamaa ambako alikuwa amezoea kwenda bila mafanikio.

Alisema taarifa za kupotea kwa binti yake walitoa katika kituo cha polisi cha Mbezi Kimara kwa KMR/RB/10362/2019.

Aliomba yeyote atakayemwona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi au kuwasiliana nao kwa namba **0754 212677, 0752396529 na 0685 561528.**

# JPM aamuru JWT Z kudhibiti ujambazi

INATOKA UK. 2

yamekuwa yakifanywa na watu wanaodhaniwa kuwa ni wakimbizi, ikiwamo kupiga watu misumari kwenye kichwa yanashangaza na kuwataka wakimbizi kufuatilia kwa karibu hali ilivyo katika nchi yao Burundi ili wanaoweza kurudi waende kujenga nchini yao.

"Sasa Burundi kumekuwa na amani. Najua wapo watu wanaonufaika kwa ninyi kuwa wakimbizi hapa, hivyo msing'ang'anie kupewa uraia wakati nchi yenu ipo.

tulishatoa uraia kwa wenzenu 120 ukiona kuna amani unarudi," alisema.

Kuhusu ujenzi wa barabara, Rais Magufuli alisema kuwa ujenzi wa barabara hiyo umegharimu Sh. bilioni 57 ambazo zimetolewa na Serikali. "Fedha zimetolewa na serikali mliyoichagua, ujenzi wa barabara za lami unagharama kubwa, kuona barabara ya lami ilikuwa ni miujiza kwa miaka ya nyuma," alisema.

Aidha, Rais Magufuli pia alitoa mwezi mmoja kwa viongozi kuhakikisha Wilaya ya Tanganyika inakuwa na Halmashauri ya Tanganyika badala ya kuitwa halmashauri ya Mpanda.

**UMEME TANESCO**

Rais Magufuli alisema Jiji la Dar es Salaam lilikuwa linanuka harufu ya petrol kutokana na kukithiri kwa matumizi ya majenerata yaliyokuwa yakisababishwa na mgawo wa umeme.

"Tulipoingia madarakani tulikubaliana kupiga marafuku ndiyo maana tuliongeza production ya umeme, kulikuwa na mgawo," alisema. Alibainisha kuwa mgawo wa umeme ulikuwa umezoeleka katika maeneo mengi, kwa kuwa kulikuwa na hujuma iliyokuwa inafanywa na baadhi ya watumishi wa Tanesco wasio waaminifu.

"Kulikuwa na watu kwenye bwawa la Mtera likijaa wanalifungulia baada ya mwezi maji yanaishi kumbe walikuwa wanalipwa fedha na watu wa jenerata, tukawatumbua wakaondoka, kutumbua siyo kubaya walikuwa wanayafungulia ili kuwe na mgawo nikamwambia waziri nenda kafukuze wote pale," alisema.

Rais Magufuli alisema serikali ilikuwa inatoa ruzuku ya Sh. bilioni 200 kwa Tanesco kila mwaka badala ya kupeleka shuleni kwasababu ya 'majipu' ambayo waliyatumbua na kwa sasa hawapeleki hata senti tano. Alisema kuwa Serikali ya awamu ya tano imekusudia kushusha bei ya umeme na viwanda vitazalisha bidhaa kwa bei ya chini hivyo itaweza kushindana kwenye soko la Afrika na dunia kwa ujumla.

## Kabendera aomba msamaha wa Rais

INATOKA UK. 4

cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama kilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, Kabendera anakusudia kuanza kufanya majadiliano na DPP kuhusiana na tuhuma zinazomkabili," alisema Olengurumwa katika taarifa yake.

"Kifungu hicho kinaeleza bayana kwamba mtuhumiwa au wakili wa mtuhumiwa au mwendesha mashtaka mkuu wa serikali, anaweza kuanzisha majadiliano na kuijulisha mahakama kuhusu nia ya kutaka makubaliano ya pamoja.

"THRDC inaamini kuwa mchakato wa makubaliano utakaoanzishwa kati ya mshtakiwa na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali utakwenda kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na kwamba matokeo ya makubaliano hayo yatakuwa ya manufaa kwa pande zote mbili," alisema.

Mwandishi huyo wa habari za uchunguzi, anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka matatu likiwamo la utakatishaji fedha wa zaidi ya Sh. milioni 173.



Msimamizi Msaidizi wa zoezi la uandikishaji wa daftari la wapiga kura katika Mtaa wa Kisukuru, Beatrice Isakwi (kulia), akifuatilia mwenendo wa uandikishaji katika mtaa huo, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# MCT yaboresha tuzo uandishi wa habari

INATOKA UK; 5

Mengine ni mchora katuni bora; uandishi wa habari za jinsia; uandishi wa habari za wazee; watoto; habari za gesi, mafuta na uchimbaji madini; habari za afya ya uzazi; habari za ubunifu na maendeleo ya watu; habari za usalama barabarani; hedhi salama na kundi la wazi.

Alisema kazi zinazotakiwa kuwasilishwa ni zile ambazo zimechapishwa kuanzia Januari hadi mwisho wa Desemba mwaka huu.

Mukajanga alisema uwasilishwaji wa kazi hizo utafanyika kuanzia Oktoba 11, mwaka huu, hadi Januari 31, mwakani.

Mtaalamu wa Mawasiliano kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Ubunifu (HDIF), Hannah Mwandoloma, ambao ni miongoni mwa wadhamini wa tuzo hizo katika kundi la tuzo za uandishi wa habari za ubunifu na maendeleo ya watu, alisema wameamua kudhamini tuzo hizo kutokana na umuhimu wake katika taifa.

Mwandoloma alisema ili nchi yoyote ipige hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi ni lazima kuwe na watu wanaofanya kazi za ubunifu.

Alisema lengo la kudhamini kundi hilo ni kuhamasisha waandishi wa habari kufichua kazi mbalimbali za kibunifu zinazofanywa katika maeneo mbalimbali ya nchi ili waweze kusikika na kusaidiwa kwa lengo la kuchangia maendeleo katika nchi.

Pia alisema uandishi wa habari za ubunifu zitawasaidia wabunifu wenyewe kutambua sera zilizopo nchini katika kufikia malengo yao.

Naye, Mwenyekiti wa Mtandao wa Wadau wa Hedhi Salama, Wilhelmina Malima, alisema wamemua kushiriki katika tuzo hizo ili kuhamasisha waandishi wa habari kuandika habari ambazo zitasaidia kuvunja ukimya uliopo katika jamii na kuongeza upatikanaji wa taarifa na kujenga miundombinu wezeshi kwa watoto wa kike.

## Mvua zasababisha madhara makubwa

INATOKA UK.; 3

kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha na kusababisha barabara ya kutoka stendi kuu ya mabasi ya wilaya kwenda eneo la Amtoco kufungwa kwa muda. Mvua hiyo ambayo mpaka sasa inaendelea kunyesha na tayari imeleta madhara makubwa kwa kubomoa madaraja na nyumba za watu ambao wamejenga katika mabonde.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, akizungumza na wananchi wa mji huo aliwataka wote waliojenga mabondeni kuondoka kabla hawajachukuliwa hatua. Mkuu huyo wa mkoa alifika eneo hilo la mto Mkurumuzi akiongozana na Ofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Muheza, Alphonce Njuu, kwa ajili ya kuwaokoa watu hao.

Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) Wilayani Muheza, Sixmund Mosha, alipeleka lori lenye winchi na kufunga kamba na kuwatupia katika maji watu hao ambao walikuwa wamekaa juu ya jiwe la daraja na hatimaye kufanikiwa kuwaokoa watu hao kwa

## Ndugu feki wakwamisha uhamishaji

INATOKA UK. 3

"Ni kweli tumetoka mbali kwa ajili ya kuja kuhamisha makaburi ya wapendwa wetu lakini kutokana na kuwapo kwa malalamiko haya na sisi tumeyasikia ,tunaomba tuwe wavumilivu ili kazi hii ikamilike bila malalamiko," alisema.

Ndahani alisema wakati wa uhakiki, kuna baadhi ya ndugu hawakupata taarifa kutokana na kuishi nje ya Mkoa wa Dodoma, hivyo baada ya kufika, walishangazwa na kuwapo kwa ndugu feki wa marehemu waliozikwa hapo. Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Chinyoya, Faustina Bendera, alisema uhakiki huo ulifanyika mara nne kwa viongozi wa mtaa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na wakajitokeza watu. Bendera alisema makaburi 79 yanatarajiwa kupitiwa na ujenzi wa miundombinu ya reli hiyo inayotarajiwa kupita hapo.

Kuhusu fidia, Mwenyekiti huyo alisema ndugu wa familia za watu waliozikwa hapo walishakubaliana na uongozi TRC kuhusu malipo na hakuna mgogoro wowote lakini wakati wa uhakiki ndio wamejitokeza ndugu feki. "Gharama za kuhamisha makaburi pamoja na kujenga makaburi zitafanywa na TRC na ndugu watalipwa fidia ya Sh.200,000," alisema.

## Waziri ataka mageuzi uzalishaji asali

INATOKA UK. 5

ambako ndiko kwenye utekelezaji, msukumo wake umekuwa mdogo.

"Ninachokiona hapa hakuna mawasiliano baina ya pande hizi mbili. Chuo cha Nyuki cha Tabora kinafanya yake huku wizarani sisi tukiamini kuwa mambo yanakwenda sawa. Hatuwezi kufika kwa mwendo huu," alisisitiza Kanyasu. Kuhusu ununuzi wa mitambo ya kuchakata asali katika mkoa wa Tabora, Kanyasu alisema kazi hiyo bado haijafanyika, hivyo akaahidi kufuatilia nini kimekwamisha. " Haiwezekani wataalamu wa kutoka TFS wanafanya upembuzi yakinifu kwa miaka mitatu lakini hakuna cha ujenzi wa kiwanda wala ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kuchakatia asali hicho leo," alisisitiza Kanyasu

Alisema mkoa wa Tabora kwa zaidi ya asilimia 70 umezungukwa na misitu ambayo wananchi wengi wanaiona haina maana kwa vile hakuna mapato wanayoyapata moja kwa moja. Kanyasu alisema moja ya vichocheo vya wananchi wa mkoa wa Tabora kuendelea kulinda misitu iliyopo ni TFS kufungua kiwanda cha kuchakata asali.

Naibu Waziri aliiagiza TFS kuajiri maofisa nyuki wa kutosha na kutoa motisha kwa maafisa hao kwa vile hata wachache waliopo, wamekuwa wakijitambulisha kuwa ni maofisa misitu. Awali, Mkuu wa Chuo cha Nyuki Tabora, Semu Daudi, alimueleza Naibu Waziri kuwa chuo hicho kimekuwa kikikabiliwa na ukosefu wataalamu wa kutosha kwa kuwa hadi sasa kina wakufunzi 15 pekee kati ya 30 wanaohitajika.

# Wananchi 6,000 kunufaika huduma za afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ZAIDI ya wananchi 6,000 kutoka vijiji vinne katika Kata ya Oldonyowas mkoani Arusha, wanatarajia kunufaika na huduma za afya na kuondokana na kutembea umbali mrefu.

Wananchi hao ni kutoka vijiji vya Losinon, Engutukoit, Kisimiri Juu na Wito watanufaika na huduma hiyo kutokana na zahanati ya kisasa iliyojengwa na wahisani kutoka Ujerumani kupitia shirika la Help for Maasai Children (HMC).

Akizungumza wakati wa kuweka jiwe la msingi na kulikabidhi jengo hilo kwa Halmashauri ya Arusha katika kijiji cha Losinon Juu, Mkurugenzi wa HMC Tanzania, Joseph Kivuyo, alisema ujenzi wa zahanati hiyo ulianza rasmi Juni 26, mwaka huu na hadi sasa umekamilika kwa asilimia 85.

Kivuyo alisema mradi wa zahanati hiyo mpaka sasa umegharimu Sh. milioni 108 na hadi kukamilika utagharimu Sh. milioni 140.

Alisema wananchi wa vijiji hivyo wamekuwa wakitembea kilometa nane hadi 12 kufuata huduma za afya. Kutokana na umbali huo, alisema wanawake wengi wamekuwa wakijifungulia njiani na wengine nyumbani, hivyo kuchangia vifo kutokana na kutokwa na damu nyingi.

"Ujenzi wa zahanati hii tumeshirikiana na Halmashauri ya Arusha ambao walitupa ramani ndipo wahisani wetu kutoka Ujerumani waliamua kutujengea baada ya kuja na kuona uhitaji mkubwa uliopo ikiwamo wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya. Tunawashukuru sana kwani wananchi wetu wataanza kunufaika sasa," alisema Kivuyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza wakati wa kuweka jiwe la msingi, aliwapongeza wafadhili hao kwa hatua ya kusaidia miradi mbalimbali katika kata hiyo ikiwamo elimu na afya. Alisema mfano huo unapaswa kuigwa na wadau wengine.

Muro aliwaahidi wananchi hao kuwaletea gari aina ya Toyota Land Cruiser kwa ajili ya kubebea wagonjwa na litakuwa linatoa huduma katika zahanati hiyo, huku akiwaahidi kutengeneza barabara inayokwenda katika zahanati hiyo ili kurahisisha huduma kufika kwa haraka kwa wananchi hao.

Naye Mfadhili wa Mradi huo ambaye ni Mkurugenzi wa HMC kutoka Ujerumani, Harald Pfeiffer, alisema ujenzi wa zahanati hiyo ni moja ya ndoto alizojiwekea muda mrefu za kuhakikisha anasaidia jamii hiyo katika elimu na afya.

Aliwataka wananchi wa kata hiyo kutumia mradi huo kwa malengo yaliyowekwa huku akiwataka kutunza miundombinu hiyo ili idumu na kutumika kwa vizazi vijavyo.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akimkabidhi msaada wa 250,000/- mkazi wa Kijiji cha Okutu, Kata ya Naberera, wilayani Simanjiro, Suzy John anayeishi kwenye mazingira magumu, katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Halmashauri yaonya watakaovuruga uchaguzi

**Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imesema haitawavumilia watendaji wa serikali waliopewa dhamana kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa ambao watakiuka sheria na taratibu kwa kushirikiana na watu wenye nia ovu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Hamisi Malinga, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake namna walivyojipanga kufanya uchaguzi huo. "Watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi huu watakaotaka kuvuruga sitaweza kuwavumilia kwa hali yoyote ile. Wanatakiwa wafanye kazi bila upendeleo," alisema Malinga.

Alisema watumishi ambao wataingia kwenye mkumbo wa kuhujumu uchaguzi huo watakuwa wanajihujumu huku akitoa mfano kuwa katika nchi yoyote mtumishi anayehujumu uchaguzi, mwenge na mitihani anashughulikiwa. Malinga alisema ni vizuri kila mmoja mwenye dhamana katika uchaguzi huo akaogopa na kuwa makini ili wabaki salama katika utumishi wa umma.

"Fedha na vifaa vimeshaletwa na maandalizi mengine yote yamekamilika. Ikitokea fedha ikapelea ya kuendesha uchaguzi huu, mimi kama ofisa masuhuli nitalazimika kuangalia kwenye vyanzo vya ndani ili uchaguzi ufanyike kwa uhuru na haki," alisisitiza.

Alifafanua kuwa hana shaka juu ya watendaji wake maana wameshapewa mafunzo ya kutosha kutoka taifa kwa ajili ya kusimamia vizuri ili wapatikane viongozi.

Mkazi wa Qash, Fatma Ramadhani, alisema wako tayari kuwachagua viongozi lakini cha msingi serikali itoe matangazo kwao ili wajue siku na maeneo ya kwenda kuwapigia kura viongozi wanaowataka.

Mkazi wa Babati, Karen Fasto, alisema uchaguzi huo ni wa muhimu kwa kuwa viongozi wanaokwenda kuwachagua ndio wako karibu na wananchi tofauti na wabunge wanaoonekana kipindi cha uchaguzi.

# Saccos zatakiwa kuajiri wahitimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VYAMA vya ushirika vya kuweka na kukopa (Saccos), vimeshauriwa kuajiri wahitimu wa chuo kikuu ili vijiendeshe kwa faida na kuachana na watendaji wasio na elimu ambao wamekuwa chanzo cha vyama hivyo kupata hati chafu za ukaguzi.

Rai hiyo imetolewa na Prof. Alfred Sife, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi, alipokuwa akifunga kongamano la kitaifa la siku mbili la Saccos lililofanyika jijini hapa.

Alisema kwa mujibu wa ukaguzi wa Saccos mwaka huu uliofanywa na Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (Coasco), vyama 300 vimepata hati safi wakati 856 vimepata hati chafu. Prof. Sife alisema hati hizo zimepatikana kutokana na vyama hivyo kuendeshwa bila ya kuwa na wataalamu, hivyo kushindwa kuandaa taarifa za hesabu na matokeo yake kuendeshwa bila ya kuzingatia taratibu za vyama hivyo.

Pia alisema chuo hicho pia kinaendesha mafunzo ya masafa kwa vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na kuendesha semina ili kuwajengea uwezo watendaji na viongozi wa vyama ambao wanategemewa kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia Saccos zao. Alisema kwa mujibu wa kaulimbiu ya mwaka huu isemayo 'Huduma kwa Jamii Kufikia Ulimwengu Ushirika Ndiyo Njia Sahihi ya Kuwezesha Kujikwamua Kiuchumi', alizishauri Saccos ziungane kwenye mwavuli mmoja ili kuwa na sauti ya pamoja na kamwe zisitegemee ushirika kuwapo iwapo zitatengana.

Akisoma risala, Mwenyekiti wa Shirikisho la Caccos nchini (Sccult), Dk. Gerevas Machimu, alisema halmashauri zinakata makato ya Saccos za watumishi lakini zinachelewesha marejesho hivyo kusababisha fursa zilizopo kudorora.

Baadhi ya Saccos, wanachama wamekuwa wakikimbilia mahakamani pindi kunapotokea mgogoro badala ya kutatua migogoro hiyo kwa kufika shirikisho la vyama vya kuweka na kukopa Saccos Scult hivyo kuathiri shughuli za ushirika.

"Lakini tunaomba tozo ya kodi ipungue kutoka asilimia 30 hadi 10 ili kuzipa Saccos unafuu. Pia Sassos zenye mtaji wa Sh. milioni 200 ndizo zitozwe kodi badala ya zile zenye mtaji wa Sh. milioni 50,"alisema.

# Waliouawa na tembo wafikia wanane

Na Godfrey Mushi, MWANGA

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na kuvamiwa na tembo katika Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro imeongezeka na kufikia wanne.

Hadi kufikia juzi jioni, katika Kijiji cha Toloha, wananchi watatu walikuwa wameuawa na tembo baada ya kuvamiwa na kushambuliwa wakiwa kwenye makazi yao wakati mwanzoni mwa wiki tembo hao waliua mkazi mmoja wa Kijiji cha Ngulu. Kwa nyakati tofauti jana, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (Tawa), Dk. Maurusi Msuha, alipokea taarifa hiyo wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Toloha na Kigonigoni.

Tembo hao wanaodaiwa kuvamia makazi ya watu na kusababisha vifo vya watu watatu na kujeruhi wengine saba, wanaelezwa kwamba wanatoka katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Hifadhi ya Tsavo ya Kenya.

Juzi, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Ngulu, Modest Mvungi, aliithibitishia Nipashe kuwa aliyepoteza maisha alijeruhiwa kwa kukanyagwa na tembo kwenye maeneo mbalimbali ya mwili wake ni Majabu Lemahuna.

Lemahuna wakati anavamiwa na tembo na kuuawa, alikuwa akichukua kuni za kupikia nje ya nyumba yake. Baadhi ya wananchi wa Kata ya Vumari, wameileleza timu hiyo kuwa kuna wimbi kubwa la makundi makubwa ya wanyama hao kuingia na kuvamia maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi kila wakati.

Tembo hao wanadaiwa kuingia kwa makundi na kuvamia mashamba, nyumba na maghala ya akiba za vyakula vya aina mbalimbali hasa nafaka kama mahindi mtama na viazi vitamu.

Mazao mengine yanayovamiwa mashambani au bustanini ni miwa, maboga, matikiti maji, matango na bustani zilizoko kandokando ya mito.




Katibu wa Chama Cha Wasioona wilaya ya Temeke, Protas Mutakyunga (katikati), akipokea moja ya fimbo 30 za kutembelea walemavu kutoka kwa Meneja Masoko na Mawasiliano wa GSM Group, Matina Nkurlu (kulia), jijini Dar es Salaam, jana, zilizotolewa msaada kupitia kampuni mama ya GALCO, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha wiki ya huduma kwa wateja. Kushoto ni mwanachama wa Chama hicho, Angela Sebastian. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamiliki mabasi walia uchakavu vituo

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

WAMILIKI wa mabasi ya abiria yanayofanya safari katika mikoa mbalimbali nchini, wameeleza kwamba hawaridhishwi na miundombinu ya vituo vya mabasi katika ngazi za wilaya kutokana na uchakavu.

Malalamiko hayo yaliwasilishwa jana na Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Enea Mrutu, wakati akichangia hoja katika kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Kilimanjaro kilichofanyika mjini hapa.

"Ukitazama stendi nyingi za mabasi katika kila wilaya, nyingi hazina viwango vinavyotakiwa. Nashauri halmashauri za wilaya zifanye ukarabati wa vituo vikubwa vya mabasi kwa sababu stendi nyingi ni chakavu na hazina hadhi ya kushusha wala kupakia abiria.

"Lakini pia, Tanroads (Wakala wa Barabara Tanzania), jengeni vituo vya kushusha na kupakia abiria katika vijiji vyote vilivyoko jirani na barabara kuu ili kuepusha ajali na usumbufu kwa abiria. Vijiji vingi vimekuwa vikubwa na watu wamesogea karibu na barabara, kwa hiyo vinastahili kuwa na vituo vya kushushia na kupakia abiria," alisema.

Mrutu alisema wamiliki wengi wanashindwa kuingiza mabasi katika vituo hivyo kutokana na ubovu wa muda mrefu, jambo ambalo limekuwa likisababisha mabasi yao kuharibika na abiria kutotaka kutumia standi hizo.

Alisema vijiji vilivyopo kando ya barabara ya kutoka Moshi mjini kuelekea jijini Dar es Salaam vikiwamo vijiji vya Chekereni, Kileo, Kifaru, Mwanga hadi mpakani mwa wilaya ya Same, vinahitaji kujengewa vituo vya kushusha na kupakia abiria.

Mrutu ambaye pia ni Diwani wa Shingatini (CCM) katika Wilaya ya Mwanga, alitoa ushauri kwa wakurugenzi wa halmashauri za wilaya kukarabati stendi za abiria na kuacha tabia ya kujenga standi mbili katika wilaya moja ili kulazimisha mabasi makubwa kuingia katika standi hizo na kulipa ushuru mara mbili.

Aidha, alisema mwongozo wa wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, unaelekeza kila basi la abiria linapaswa kuingia stendi kushusha au kupakia abiria na kulipa ushuru wa halmashauri husika na si kukamata na kulazimisha mabasi hayo kuingia kila kituo na kulipa ushuru.

"Taratibu zipo wazi kabisa na zinaelekeza mabasi ya mikoani kulipa ushuru wa halmashauri kila stendi wanapokuwa na abiria wa kupanda basi au kushusha na si kulazimisha mabasi kuingia stendi," alisema Mrutu.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alitoa wito kwa wafugaji kuacha tabia ya kuchunga mifugo yao kando kando ya barabara kuu ili kuepusha ajali zisizo na ulazima.

Pia Mghwira aliagiza Kikosi cha Usalama Barabarani kuanza kuyakamata na kuyatoza faini mabasi ya abiria yasiyokuwa na vifaa vya kutupia takataka na fedha zitokanazo na faini zinunue mapipa maalumu ya kuhifadhia taka na abiria kupata vyoo vya kujisitiri.

## RC aagiza msaada wa NMB kuboresha elimu

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameagiza misaada yote iliyotolewa na Benki ya NMB inayogharimu Sh. milioni 85 ielekezwe katika halmashauri sita kwa ajili ya kuboresha huduma za afya na elimu.

Pia ametaka wadau wa maendeleo, taasisi za kifedha na wahisani wanaotaka kutoa misaada yeyote ya kijamii, kupata kwanza ushauri katika ofisi yake kuhusu nini ambacho kinahitajika zaidi katika mkoa wa Kilimanjaro.

Mghwira alitoa maelekezo hayo jana muda mfupi baada ya makabidhiano ya vifaa mbalimbali vya elimu na afya, vilivyotolewa na NMB.

"Kwa sasa hitaji letu kubwa ni matundu ya vyoo kwa walimu na wanafunzi walioko katika shule za msingi na sekondari. Sasa ukitaka kutusaidia tuulize kwanza ili tukwambie utusaidie kitu gani na si kuleta kile ambacho kina afadhali," alisema Mghwira.

Vifaa vilivyokabidhiwa kwa mkuu huyo wa mkoa ni madawati, mabati, mashuka na vitanda.

Pamoja na mambo mengine, mkuu huyo wa mkoa aliitaka menejimenti ya NMB kuanza kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wateja wao ili kuboresha utoaji wa huduma zao badala ya kuruhusu wateja kwenda kulalamika katika ofisi yake.

Benki hiyo imetoa msaada wa vifaa vya Sh. milioni 10 kwa Halmashauri ya Hai, Siha, Sh. milioni 10, Moshi Sh. milioni tano, Rombo Sh. milioni 15, Same Sh. milioni 30 na Mwanga Sh. milioni 15.

Awali, Mkuu wa Idara ya Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo, alimweleza mkuu huyo wa mkoa kwamba kwa sasa wamesogeza huduma za kibenki karibu na wateja wao na kwamba wako tayari kutekeleza maelekezo yake kwa uharaka zaidi.

Alisema msaada huo ni sehemu ya mchango wa benki hiyo kwa jamii inapofanya shughuli zake ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki kwa mteja.





Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Benilith Mahenge (kushoto), akijiandikisha kwenye daftari la wapiga kura la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika kituo cha Nyerere, eneo la Kilima, jijini Dodoma jana. Kulia ni Mwandikishaji wa kituo hicho, Tishio Kipingi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbolea tani 45,000 kuingiza nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Ushirika cha Wazalishaji na Wasambazaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo (TADCOS), kinatarajia kuingiza tani 45,000 za mbolea kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

Mboleo hiyo yenye thamani ya Sh. bilioni 38, kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo kwa mujibu wa Mwenyekiti wa chama hicho, Gerald Mlenge .

Akizungumza katika semina ya kuwajengea misingi ya uongozi katika ushirika iliyoendeshwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Mlenge alisema mbolea hiyo inatarajia kuwasili nchini kuanzi mwezi ujao , Novemba 20 .

Aliahidi kuwa itasambazwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya msimu wa kilimo unoanza sasa.

Alisema mbolea hiyo itapelekwa kwa wakati ili kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano ambayo inaweka msisitizo katika sekta ya kilimo. "Mbolea hiyo itawasili Novemba 20 na itaanza kusambazwa mara moja kwa wakulima mara itakapowasili, lengo letu ni kuona wakulima wote katika kanda zote wanapata mbolea kwa wakati kulingana na msimu wa mvua katika kanda husika,"alisema.

Aliishukuru serikali kwa kuwapa jukumu la kuagiza mbolea hiyo kwa ajili ya wakulima na kuahidi jukumu hilo watalifanya ipasavyo na kwa wakati kama inavyotakiwa. Aliomba serikali kufanya mchakato wa kuwalipa fedha za malimbikizo ya madeni ya mawakala hao ili ziweze kuwasaidia katika shughuli mbalimbali ikiwamo usambazaji wa bidhaa zao kwa wakulima.

Makamu Mwenyekiti wa TADCOS, Idd Mbago, alisema kama viongozi wamezingatia maagizo yaliyotolewa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo ya kuzingatia mambo matatu katika uagizaji mbolea hiyo. Alitaja mambo hayo kuwa ni mbolea kuwasili kwa wakati,ubora na gharama nafuu kwa mkulima ili kila mmoja waweze kumudu kununua.

Aidha, alisema wasambazaji wa pembejeo hizo za kilimo wakulima wategemee huduma bora na za kuridhisha kutoka TADCOS ambayo itawasilisha pembejeo za kilimo kwa wakati ili wakulima waendeshe kilimo chenye tija kwa jamii inayowazunguka.

Aidha, akizungumza kwenye mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo wa Tume ya Ushirika jijini Dodoma, Dorothy Kalikamo alisema mafunzo waliyowapa wanaamini yatawasaidia kwa kiasi kikubwa kuendesha chama hicho cha ushirika kwa ufasaha huku wakizingatia misingi ya ushirika. Aliagiza chama hicho kuendeshwa kwa kufuata sheria na kanuni ya vyama vya ushirika jambo ambalo litawasaidia kutotetereka.

# Wataka udhibiti watoto sokoni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa masoko jiji la Dodoma, wameagizwa kuwadhibiti watoto walio chini ya miaka 18 wanaobeba mizigo kwenye masoko kwa kuwa ni kinyume na sheria ya watoto.

Agizo hilo lilitolewa jana na Ofisa Masoko Jiji la Dodoma, James Yuna, alipokuwa akizungumza na viongozi wa umoja wa wabeba mizigo wa soko la Majengo jijini hapa, kufuatia kubainika kuwapo kwa watoto wanaojishughulisha na kubeba mizigo ya wateja.

Alisema kitendo cha kuwaruhusu watoto hao kubeba mizingo ni kukiuka sheria ya haki ya mtoto ambayo haipaswi mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18 kubeba mizigo.

"Hivyo ninaagiza uongozi wa soko na ule wa wabeba mizingo kuhakikisha watoto walio chini ya miaka 18 hawaingii ndani ya soko na kubeba mizigo. Alionya kuwa aidha, wasishushe mizigo kwenye magari au kuwabebea wateja wanaoingia kupata huduma,"alisema.

Vile vile, aliagiza viongozi wa umoja huo kuvaa sare walizokabidhiwa ambazo zina nembo na namba mgogoni ili waweze kutambuliwa na wateja wanaohitaji huduma zao za kuwabebea mizigo.

Alisema kuwa kumekuwepo na tabia kwa baadhi ya wabeba mizigo kwenye masoko ambao siyo waaminifu.

"Tayari ninayo taarifa ofisini kwangu kuwapo kwa baadhi ya wabeba mizigo ambao si wanachama kwenye umoja wenu ambao wakipewa mizigo hiyo wanatokomea nayo suala ambalo linachafua sifa ya uaminifu mlionao ninyi mlio waminifu,"alisema.

Aliwaagiza kushirikiana na uongozi mzima wa masoko ili waweze kuwabaini wezi hao wa mizigo.

Katibu wa umoja wa wabeba mizigo soko la Majengo, George Eleutery, alisema kuwa uongozi wao utahakikisha unatoa ushirikiano kwa lengo la kuwabaini wanaobeba mizingo ambao siyo waaminifu na wale wasiokuwa na sare. Alisema umoja huo utahakikisha usalama wa mali za wateja zinalindwa na hata pale inapotokea uharibifu watakuwa tayari kutoa taarifa kwenye vyombo husika ili wateja wanaotumia soko hilo wawe na imani na huduma wanazopatiwa.

## Takukuru yawapa somo wapiga kura

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imewataka wananchi kutumia haki yao ya msingi kuchagua viongozi bora watakaosimamia miradi ya maendeleo.

Aidha, wamehimizwa katika serikali za mitaa wawachague wagombea wanasiopenda rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Taasisi hiyo mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wananchi wanapaswa kuchagua viongozi wenye weledi ambao watasaidia kusimamia miradi ya serikali iliyopo na si kuchaguana kwa kujuana.

Alisema hakuna sababu ya wakazi wa maeneo tofauti kukubali kushawishiwa kuchagua viongozi kwa kupokea rushwa ndogo ndogo na kwamba kinachotakiwa ni kuangalia kiongozi anayestahili na ambaye ataweza kusimamia miradi ya serikali kwa weledi.

"Nawaomba wananchi tuchague viongozi kwa matakwa yetu tusirubuniwe na rushwa tukachagua viongozi wapinga maendeleo na wapendwa rushwa," alisema Kibwengo.

Alisema lengo lao ni kuona kila mtaa unapata kiongozi sahihi ambaye anaweza kuiongoza jamii inayomzunguka ikiwamo kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayofanywa na serikali ya awamu ya tano.

Alifafanua zaidi kuwa serikali ya awamu ya tano inafanya jitihada kubwa za kuinua uchumi wa wananchi kupitia miradi inayotekelezwa hivyo wao nao wanapaswa kutoa ushirikiano ili miradi hiyo isimame kama inavyotakiwa.

"Takukuru hatutakuacha endapo tutakubaini una viashiria vya rushwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yako," alisema Kibwengo.

Kibwengo alisema katika robo ya mwaka huu mwezi Julai hadi Septemba hali ya rushwa kwenye kata, mitaa na vijiji imeonekana ipo juu na haileti picha nzuri kwa jamii.

Hata hivyo, alisema Takukuru inaendelea kutoa elimu kuhusu kupinga rushwa katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha jamii yote inapata uelewa juu ya suala zima la kukataa rushwa.

Alisema elimu hiyo wanaitoa kupitia klabu mbalimbali ambazo zimeanzishwa ili kusaidia kuielimisha jamii kuhusiana na madhara ya rushwa hususan katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaofanyika mwezi ujao (novemba 24).





Baadhi ya wakazi wa Kata ya Bugoji, jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara wakishirikiana na mafundi kujenga msingi kwa ajili ya madarasa ya Sekondari mpya ya Kumbukumbu ya Dan Mapigano, juzi, ambayo inatarajia kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# SMZ yapania mapinduzi ya kilimo

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali imejizatiti kuendeleza kwa vitendo mapinduzi ya kilimo kwa kuwapa taaluma ya kilimo bora wakulima, wafugaji na wavuvi.

Akifungua juzi maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani, yaliyofanyika katika viwanja vya Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba, alisema katika kutekeleza azma hiyo, serikali itaendelea kutoa huduma za matrekta na pembejeo za kilimo.

Dk. Shein alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara ili kuwawezesha wafanyabiashara kuingiza na kuuza zana, vifaa na pembejeo za kisasa kwa wakulima kwa bei nafuu.

Aidha, Dk. Shein aliwataka wakulima kulima kwa kuzingatia matumizi ya mbinu za kisasa za kilimo na kufuata maelekezo ya wataalamu na kutaka kuwapo matumizi bora ya pembejeo za kilimo, mbolea na wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea.

Ili kufanikisha azma hiyo, alitaka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhakikisha inakuwa na mipango na mikakati madhubuti katika kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwasaidia wananchi ili kuwa na mwamko wa kutumia teknolojia bora za kilimo katika mazao mbalimbali.

"Maarifa watakayopata wananchi kupitia maonyesho haya yatawasidia kupata mbinu mpya za kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuongeza tija", alisema.

Aidha, alisema kupitia maonyesho hayo, wananchi watapata fursa ya kuzijua taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji pamoja na wajasiriamali na hatimaye kusaidiwa.

Alisema wananchi watajifunza na kuitumia elimu watakayoipata ili kuongeza uzalishaji katika shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji, hivyo kukuza uchumi na kujiongezea kipato.

Kuhusu uendelezaji kilimo cha mpunga, Dk. Shein alisema kuna mafanikio makubwa kutokana na kuongezeka kwa mavuno yaliyoanza kupatikana na kusema hivi sasa serikali imejielekeza katika mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kupitia mkopo wa Dola milioni 50 kutoka Benki ya Exim ya Jamuhuri ya Korea.

Alisema mradi huo utatekelezwa katika mabonde matano yanayozalisha mpunga ya Cheju, Kilombero, Bumbwisudi, Mkwararani na Mlemele, hatua itakayopanua wigo wa kilimo cha mpunga kutoka ekari 810 hadi 2,397. Kutokana na ongezeko hilo, alisema kuna matarajio makubwa ya kuongezeka kwa mavuno kutoka wastani wa tani 31,000 za mchele hadi tani 70,365, hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza bidhaa hiyo.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema mwelekeo wa sekta ya kilimo ni kuongeza uzalishaji na usarifu wa mazao ili kuongeza tija.

Aliipongeza serikali kwa juhudi za kutoa kipaumbele katika sekta ya kilimo, ili kuona uzalishaji wa chakula onaongezeka na kuleta tija kwa jamii.

# Waziri ataka NGO kufuata sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ASASI za kiraia zimetakiwa kutumia fursa iliyotolewa na serikali ya kuanzishwa kwazo ili kurahisisha kupatikana kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Akifungua juzi Jukwaa la Wakurugenzi wa Asasi za Kiraia Zanzibar, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, alisema asasi za kiraia ni miongoni mwa wadau wakuu wenye dhamana ya kuwaunganisha wananchi na serikali katika kusimamia shughuli za maendeleo.

Khamis alisema asasi hizo pia zina wajibu mkubwa wa kuchangia katika shughuli za maendeleo yanayohusiana na masuala ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya wananchi.

Naibu waziri huyo aliwataka viongozi wa asasi hizo kutumia fursa hiyo katika kipindi hiki cha mfumo wa madaraka mikoani kuhakikisha wanasaidia kutatua matatizo ya kijamii.

Aidha aliziasa baadhi ya asasi zinazokwenda kinyume na malengo ya kazi zao kubadilika kabla ya serikali kuzichukulia hatua.

Khamis alisema serikali inaahidi kuweka mazingira mazuri ili asasi za kiraia zishiriki bila vikwazo lakini lazima zijue wajibu kuwa wana jukumu kubwa la kushirikiana na serikali katika ku waletea mae ndeleo wananchi.

"Niwape hongera kwa kutumia jukwaa hili kufanya tathmini ili kujua mafanikio, changamoto na baadaye kutoa mapendekezo ambayo yakifanyiwa kazi yataimarisha ubia uliopo katika asasi za kiraia," alisema.

Naye Mrajis wa Asasi za Kiraia Zanzibar, Ahmed Khalid Abdalla, alizita asasi hizo kujipima utendaji wa kazi zao na kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya jamii.

Alisema hadi sasa kuna baadhi ya asasi za kiraia ambazo hazijaelekeza nguvu zao katika kutatua changamoto mbalimbali za kijamii.

"Kwa mfano kwa upande wa elimu iliyogatuliwa hivi karibuni, tuna uchache wa madarasa ya kusomea na pia baadhi ya watoto wanatembea umbali mrefu kufuata elimu ya awali" alisema.

# Watalii watolewa hofu usalama wao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, amesema serikali imekuwa ikifanya mambo mengi kuhakikisha usalama wa watalii na wananchi kwa jumla unaimarika.

Kutokana na azma hiyo, amesema serikali imeanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumu (JKU) na kufunga kamera zinazoweza kurikodi matukio yoyote ya uhalifu yanayoweza kujitokeza.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar (Zati), waziri huyo alisema ni wakati sasa jumuiya hiyo iwe mwavuli wa kuzibeba taasisi zingine zinazojishughulisha na sekta ya utalii ili iwe rahisi kupanga mikakati mizuri zaidi ya kuimarisha sekta hiyo.

Kombo alisema serikali imekuwa sikivu kusikiliza maoni na ushauri wa wawekezaji wanayotoa kutaka kuimarishwa kwa miundombinu na maeneo mengine ambayo ni muhimu wa ukuaji utalii wenye tija.

Aidha, aliutaka uongozi wa jumuiya hiyo kufanya kazi ya ziada kupata wanachama wapya ambao ndio msingi wa mafanikio katika mkusanyiko wowote unaofanya shughuli za kiuchumi na biashara kama ya utalii.

Waziri alisema kuwa na wanachama wengi kutaiwezesha jumuiya kukusanya ada ambazo zitatumiwa katika kufidia nguvu, wakati na fedha zinazotumika kuendeshea jumuiya.

Waziri Kombo alisema si busara kuwapo watu au jumuiya zinazofanya kazi za kitalii ambazo zinanufaika na Zati kwa namna yoyote lakini hawamo katika orodha ya wanachama wanaolipa ada.



**WEUSI WANGU ULININYIMA RAHA, SASA NINA FURAHA**
UK.19

JUMAMOSI OKTOBA 12, 2019

BURUDANI TELE



# AKINUSURIKA Meninah bahati yake

## BASI SAWA




## Baby ya Kesy Material we acha tu

Msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Kasy Material, amefanya kazi nzuri baada ya kuachia kava ya wimbo 'Baby' wa Joeboy kutoka Nigeria.

Msanii huyo amerudia wimbo huo kwa lugha ya Kiswahili na kuufanya kuwa na mvuto wa kipekee.

Mashabiki wa muziki waliosikiliza wimbo huo wamemwagia sifa Kesy material kutokana na kufanya kazi hiyo nzuri.



## Mwana FA atoa nasaha nzito

MKALI wa misemo katika muziki wa Bongo-fleva, Mwana FA, amesema wasanii chipukizi wanayakiwa kuheshimy kazi zao ili wapaye mafanikio.

Akizungumza na BT, amesema kuna tabia ya wasanii wanaoibuka kutojiamini na badala yake wanadhani wanamuziki wakubwa watawatoa.

"Kila msanii chipukizi afahamu kwamba kuheshimu kazi na kujiamini ni mambo pekee yatakatomfanya kuwa na mafanikio katika sanaa na si vingine," amesema Mwana FA.



# AKINUSURIKA Meninah bahati yake

AKINUSURIKA bahati yake! Ndivyo wanavyosema baadhi ya watu waliokerwa na msamii wa muziki wa Bongo Fleva, Menina, ambaye video yake ya faragha imesambaa katika mitandao ya kijamii.

Kauli hiyo inafuatia Baraza la sanaa Tanzania (Basata) kuamua kuingilia kati sakata hilo na kumtaka msanii huyo kwenda ofisini jana kwa ajili ya mahojiano.

Katika barua ya wito imesisitiza kwa chombo hicho kama msimamizi mkuu wa sanaa, haitavumilia kuona msanii anakiuka heshima na maadili ya Mtanzania.

Imesema katika kuangalia mitandao ya kijamii, imeona video na picha za msanii huyo akiwa mtupu ikisambaa jambo ambalo ni kintume na utaratibu. Watu mbalimbali wakiwemo mastaa walikemea kiyendo hicho wakisema inakiuka utu na kwenda kinyume na maadili ya Kitanzania.

Waliitaka serikali kuchukua hatua kali badala ya kukemea tu na kumpa umaarufu mtu husika.

Hata hivyo, Menina amekana kuhusika kusambaza video hiyo akiamini kuna watu wachache ambao wameamua kuisambaza ili wamchafue.

Hata hivyo, ameomba radhi watanzania kutokana na kadhia hiyo kwani hata yeye imemuumiza sana.

## INSTA-TWITTER





**Mwigizaji** mashuhuri nchini Tanzania alipoulizwa siri ya ndoa yenye furaha na amani kwa miaka yote hiyo tena wakiwa na mtoto mmoja alijibu hivi. "Mke kusamehe ujinga wa mumewe, Na mume kupuuzia upumbavu wa mkewe " Tubebeane vilema vyetu maana hakuna ndoa ya malaika, bali ya binadamu wenye kasoro-**Mwijak**



**Kamari** sio dhambi, ila dhambi kucheza kamari-**Madebe Lidai.**



## Giggy Money ampigia saluti Jokate

MWANAMUZIKI na mpambaji wa video za muziki wa Bongofleva, Giggy Money, amemfananisha Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegele, kama raisa wa vijana kutokana na utendaji wake wa kazi.

"Kwa sasa naweza kusema ni rais wa vijana, nimekuja kuonana naye na nitazidi kuja hapa" amesema.

Muimbaji huyo ameyasema hayo mapema juzi muda mchache baada ya kufanya mazungumzo na kiongozi huyo.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

UNASEMAAA...

# Odemba kuna kitu kinamnyima raha

MWANAMITINDO wa Kimataifa, Miriam Odemba, amesema licha ya kupata mafanikio lakini hana furaha kwa kutokuwa na elimu ya kutosha.

Akizungumza hivi karibuni, Miriam amesema katika kazi yake ya mitindo ametembea nchi nyingi duniani na amefanya mambo mengi yenye mafanikio, lakini anapofikiria kwa nini amekosa elimu anajisikia hana furaha.

"Ukweli nimetembea duniani kote, nimepata mafanikio mengi lakini kuna jambo nikikumbuka nakosa raha, nalo ni kukosa elimu," amesema Odemba.



## INSTA-TWITTER

Tuffollow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Wallah** siamini kama leo tumetimiza mwaka. Uliponitoa na nilipo sasa nakuheshimu sana mwanamke wangu. Mmebaki wachache sana duniani wanawake wenye heshima na upendo na kujali. Bustani pekee niliyoiwagilia mwenyewe. Wala hatumwagilii watu wawili. Nakuzimia sana-**Dogo Janja.**



**Poteza** smartphone, halafu ununue simu ndogo ya toshi. Hapo ndipo utakapogundua kuwa una marafiki watatu tu-**Roma Mkatoliki.**



**Mapenzi** Ulaya tu, Afrika ni biashara. Ukiona mwanamume amepoti hivyo, unadhani nini kimemtokea?-**Mkude Simba.**

## Kuumbe!


WASTARA


MONALISA


DOGO JANJA

# Mastaa walioana Bongo

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI Patrick Balisidya alimtungia wimbo dada yake Dyanabo Balisidya alipoolewa. Wimbo wake ukawa maarufu sana. Unaendelea kupigwa hadi leo kwenye sherehe za harusi. Unaitwa 'Kuoana ni Jambo la Sifa.' "Kuoana ni jambo la sifa. Natena ni jambo la fahari kubwa katika historia ya binadamu." Ni baadhi ya mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo. Kuoa au kuolewa hakujalishi kuwa wewe si staa au mtu wa kawaida. Ni jambo muhimu kwa binadamu mwenye akili timamu na aliyekamilika. Hapa Bongo wapo mastaa waliooa watu ambao si maarufu kabisa. Wana sababu zao kwa sababu mapenzi hayachagui. Kuna mastaa ambao hawajaoa, lakini wana mapenzi na mastaa wenzao. Wanajulikana. Lakini pia kuna mastaa ambao wamefunga ndoa na mastaa wenzao.

Hawa ndiyo tutawaangalia leo. Haijalishi kuwa kwa sasa wameachana, kifo kimewatenganisha, au bado wapo kwenye ndoa hadi leo.

**TYSON NA MONALISA**

Ndoa ya mastaa iliyotikisa miaka ya nyuma Bongo ilikuwa kati ya muigizaji aliyekuwa kwenye chati wakati huo, mwigizaji Yvonne Cherrie na mtayarishaji na mwongozaji wa filamu nchini kutoka Kenya George Otieno maarufu kama 'Tyson'.

Awali ilionekana ni kama ni vigumu kwa mastaa kuoana, lakini kwa ndoa hiyo, ikaonekana si jambo la ajabu na inawezekana. Ilifungwa mwaka 2001.

Kwa bahati mbaya walitengana mwaka 2005 na kupena talaka rasmi mahakamani mwaka 2012. Tyson alifariki dunia mwaka 2014 kwa ajali ya gari.

**SAJUKI NA WASTARA**

Ndoa nyingine ya mastaa iliyotikisa Bongo miaka ya nyuma ilikuwa ni kati ya waigizaji nyota kabisa nchini, Juma Kilowoko maarufu kama Sajuki na Wastara Juma.

Walioana mwaka 2009 na kuishi maisha ya amani, upendo na utulivu. Ni ndoa ambayo ilivunjwa na kifo. Kama ahadi inayotolewa na wanandoa kuwa 'tuishi hadi kifo kitutengenishe', ndivyo ilivyokuwa na kwa wanandoa hao. Ni baada ya Sajuki kufariki dunia mwaka 2013.


FLORA MVUNGI

**DOGO JANJA NA IRENE UWOYA**

Kwa miaka ya hivi karibuni kuliibuka ndoa moja matata iliyokuwa gumzo mitaani, kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii.

Ni kati ya Dogo Janja ambaye ni mwimbaji wa muziki wa kizazi kipya na mwigizaji maarufu nchini aliyewahi pia kugombea mashindano ya ulimbwende nchini, Irene Uwoya.

Walioana mwaka 2017. Hata hivyo ndoa hiyo ilidumu miaka miwili tu. Japo mwaka 2018 kulizuka tetesi hizo, lakini mwanzoni mwa mwaka huu, mambo yote yakawa hadharani. Hata hivyo wanaingia kwenye orodha ya wasanii maarufu waliowahi kufunga ndoa.

**H BABA NA FLORA MVUNGI**

Ndoa inayofuata ni kati ya mwimbaji mwingine ya bongo fleva, H Baba aliyefunga ndoa na mwigizaji maarufu nchini Flora Mvungi. Ilifungwa mwaka 2013. Kuna maneno mengi yanasemwa kwa sasa kuhusu ndoa hii. Wengine wanadai imevunjika, lakini H Baba mwenyewe amesema ipo.

Vyovyote itakavyokuwa lakini hii nayo inaingia kwenye rekodi ya ndoa za mastaa kwa mastaa nchini Tanzania.

**MARLAW NS BESTA**

Hawa wote ni waimbaji. Waliwahi kutamba huko nyuma, wakati ndiyo kwanza bongo fleva inachukua kwenye chati yake.

Baada ya ndoa yao kufungwa kuliibuka ukimya mkubwa. Hata hivyo Marlaw ameibuka juzi na kusema ndoa yake ipo kama kawaida na anaendelea kuishi na mkewe kwa amani na utulivu.

Hii ndiyo ndoa ya mastaa kwa mastaa ambayo uhakika kwa moja kwa moja unaonyesha kuwa bado inaishi.


IRENE UWOYA



## URAIS UMEMPONZA

# Bobi Wine sasa kawa kipusa

URAIS umemponza! Ndivyo unaweza kuelezea kwa kile kinachomkuta mwanamuziki na Mbunge wa Kyadondo mashariki, Robert Kyagulani maarufu Bobi Wine, ambaye kila mara anakumbana na vikwazo kutoka jeshi la polisi.

Katika tukio la hivi karibuni, mwanamuziki huyo alizingirwa na polisi akiwa nyumbani kwake kuzima tamasha la muziki alilolliandaa kwa ajili ya kusherehekea siku ya Uhuru wa nchi hiyo.

Naibu inspekta jenerali wa polisi, Asuman Mugyenyi alitetea hatua hiyo akisema waandalizi wa tamasha hilo walishindwa kuweka usalama uliohitajika.

Kulingana na BBC, kamanda huyo alidai tamasha hilo halikuwa na watoa huduma ya afya, pia hakukuwa na udhibiti wa idadi ya watu na usalama wao jambo lililosababisha kulifuta tamasha hilo.

Tamasha hilo lilikuwa liende sambamba na maadhimisho ya siku ya Uhuru inayoadhimishwa Jumatano katika wilaya ya mashariki ya Siroko.

Mgombea huyo wa urais ni mkosoaji mkubwa wa rais Yoweri Museveni na anajionyesha kuwa mpiganiaji wa watu masikini.

Kufutwa kwa tamasha hilo kunajiri baada ya siku chache serikali kupiga marufuku uvaaji wa kofia ya rangi nyekundu ambayo Bobi Wine amekuwa akiitumia kama nembo ya vuguvugu lake.

Chini ya sheria mpya iliyotangazwa mwezi uliopita, kofi hiyo kwa jina Red Beret inafaa kuvaliwa na jeshi la – UPDF.

Mwanamuziki huyo amechapisha picha katika mtandao wake wa twitter akionyesha maofisa wa polisi wakizingira nyumba yake na kuweka vizuizi katika barabara iliokuwa ikielekea katika nyumba yake inayofahamika kama One Love Beach Busabala.

Nyota huyu wa mtindo wa Afrobeats aliingia katika taaluma ya muziki katika miaka ya 2000, na anaelezea kipaji chake kuwa ni cha kuelimisha na kuburudisha. Mojawapo ya vibao vyake vya awali Kadingo, inahusu usafi wa mwili.

Alizaliwa 12 Februari 1982, Bobi Wine na alikuwa na miaka minne pekee Museveni alipoingia madarakani mwaka 1986.



# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA




1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



TUMA MESEJI - 0773 477 311




# Hulka; Ujanja mwingi mbele kiza

**Na Adam Fungamwango**

MTU anayeza kujifanya mjuaji na kufanya mambo mengi ya kujifurahisha nafsi, lakini ni mambo mabaya na najisi mbele ya Mwenyezi Mungu, lakini kumbe huwezi kujua mbele ya safari hatima yake itakuwa nini.

'Hulka' ni flamu ambayo inamhusu dada mmoja aliyelazimisha kuolewa na mwanamume, lakini lengo haikuwa ndoa. Alikuwa na kitu tofauti moyoni mwake.

Kwa sababu mwenzake wote wameolewa? Kuondoa mkosi? Au awe na kwa kujishikiza?

Waliocheza filamu hii ni Madebe Lidai, Mohamed Nurdin maarufu kama Chekibudi, Suleiman Barafu, Anwar Nassor na wengineo.

Inaanza kuonyesha kuwa Anwar anakwenda nyumbani kwa rafiki yake Madebe. Hamkuti, lakini anamkuta mkewe. Anamuuliza shemeji yake kama ana mwanamke au la jambo ambalo linamshangaza Anwar.

Anamjibu shemeji yake kuwa alikuwa na mwanamke, lakini kwa sasa wameachana.Hidaya ambaye ni mke wa Medebe anamwambia shemeji yake Anwar kuwa kesho wakutane kwenye njia ya kwenda kisimani kuna kitu anataka kumwambia, wanakubalia.

Wanakutana kesho yake, Hidaya anamwambia shemeji yake kuwa anampenda. Anwar anashangaa na kumuuliza shemeji yake kwa nini anataka kumsaliti mumewe?

Anamjibu kuwa yeye hahofii hilo, ila kwa sasa anachotaka wakubaliane wawe wapenzi. Inakuwa hivyo. Hata hivyo wakati wanazungumza kuna mtu ambaye kidogo ana matatizo ya akili 'chizi wa mtaa' alikuwa akiwasikia.

Baada ya miezi sita Hidaya anapata ujauzito. Mumewe Madebe anafurahi sana na akuahidi kumtafutia zawadi kubwa mkewe kama atajifungua salama.

Siku moja Madebe anaangusha pochi, inayookotwa na chizi. Bila kuangalia ndani kuna nini anamrudishia Madebe nyumbani kwake. Anamshukuru, lakini chizi huyo anaondoka akiwa anaongea maneno ya mafumbo ambayo Madebe hajui maana yake.

Hidaya anaomba ruhusa kwenda kijijini kwao kumuona shangazi yake mgonjwa.

Anaporuhusiwa, badala ya kwenda huko alikoomba anaenda kwa hawara yake Anwar, akipika na kupakua bila kujali watu wanaomuona.

Baada ya wiki moja kupita, Madebe anapokea taarifa za msiba kutoka ukweni kuwa shangazi yake amefariki, hivyo anatakiwa kumtaarifu pia na mkewe waende mazishini.

Madebe hashangazwi na taarifa za kifo, ila kuambiwa amtaarifu mkewe ambaye tayari anajua yupo huko.

Mwisho wa siku anaamua kwanza kwenda kwa rafiki yake Anwar ili akamuelezee jambo hili kabla hajaondoka.

Alipofika, alishangazwa kuona nguo za mkewe zikiwa zimeanikwa nje, lakini alipogonga hodi mkewe alitoka pamoja na rafiki yake Anwar.

Hata hivyo, chochote walichotegemea sicho. Madebe aliwasamehe na kumchukua mkewe akarudi naye nyumbani.

Siku chache baadaye Anwar anajiua kwa kunywa sumu kali, akihofia kuwa huenda Madebe atalipa kisasi.

Hidaya naye anakamatwa kutokana na makosa aliyoyafanya nyuma, kabla hajaolewa na Medebe. Akiwa gerezani anajifungua na Madebe kwenda kumchukua mtoto ambaye kiuhalisia si kwake bali wa marehemu Anwar.

Hata hivyo, Madebe anapewa mamlaka ya kumchukua mtoto huo awe wa kwake.



## 'WEUSI WANGU'

# Ulininyima raha, sasa nina furaha

MSHINDI wa tuzo ya Oscar, Lupita Nyong'o, ameamua kupasua nyongo kutokana na watu wanavyombagua kutokana na rangi yake kuwa nyeusi sana.

Lupita ambaye ni mwigizaji na mwanamitindo maarufu, amesema hata katika familia yake walikuwa wakimbagua kwa rangi yake jambo ambalo lilimnyima furaha.

Akizungumza katika kipindi cha BBC, mrembo huyo ameeleza suala la ubaguzi wa rangi kwa watu weusi lipo duniani kote na ametolea mfano hata katika vyombo vya habari vikubwa wanawatafuta wanawake wenye ngozi nyeupe.

Akizungumzia maisha yake, amesema kwa upande wake alikuwa akitambulika kwa weusi wake tangu alipokua mdogo nchini Kenya.

Amesema kutokana na rangi yake kuwa nyeusi sana mdogo wake wa kike ambaye ana ngozi nyeupe alikuwa akiitwa mrembo

"Mdogo wangu wa kike alikua akiitwa mrembo kwasababu yeye si mweusi sana kama mimi. Nilijiona sina thamani", amesema Lupita.

Lupita ameonya kwamba kitendo cha kumtambua mtu kwa rangi yake kuwa mweusi sana au mweupe sana ni mwanzo wa ubaguzi wa rangi.

Hata hivyo, jambo linalomsikitisha ubaguzi huo unatoka katika nchi za Kiafrika ambapo wengi zaidi ni weusi.

Amefananisha hali hiyo sawa na ukoloni wa kifikra ambao unatakiwa kukomeshwa.

"Ulimwengu unaofadhili ngozi nyepesi juu ya ngozi nyeusi, hili jambo linanipa hofu na kuniogopesha".

Lupita ambaye wazazi wake wanatoka nchini Kenya, hivi sasa anaishi Marekani na kuendesha shughuli zake za urembo na uigizaji.



# Wizikid kumbe una upendo

KWELI usanii sio vita! Ndivyo anavyotoa somo Wizkid, baada ya kuwataja wanamuziki wenzake Davido, Burna Boy na Rema kama vinara wa muziki nchini Nigeria.

Akizungumza na BBC Radio, Wizkid ambaye alivunja rekodi kwa kutumbuiza ukumbi wa Arena Birmingham, Uingereza amesema wanamuziki hao anawapenda kutokana na kazi zao nzuri.

"Ndiyo kila mtu anampenda mtu mwingine, mimi nampenda kila mtu, namsaidia kila mtu," amesema Wizkid.



## Tekashi sasa kuhukumiwa Desemba

JAJI wa mahakama moja nchini Marekani, amekubali kutaja tarehe mpya ya kutoa hukumu dhidi ya rapa Tekashi, ambaye anakabiliwa na kesi ya matumizi ya nguvu.

Jaji Paul Englemayer amekubali kutoa hukumu hiyo Desemba 18, 2019, badala ya Januari 24, 2020 tarehe iliyopangwa awali.

Walinzi wake Ellison na Mack wote walihukumiwa kutokana kuwa na makosa mengi. Ellison alikutwa na hatia ya utekaji nyara pamoja na kupanga njama na kushambulia kwa silaha hatari. Mack alipatikana na hatia ya utumiaji na usambazaji wa madawa ya kulevya.

## Kelvin Hart arejea kazini

MWIGIZAJI Kevin Hart amerudi tena kazini baada kuwa nje kwa wiki kadhaa kufuatia kupata ajali mbaya ya gari. kutokana na kupata majeraha ya kichwa.

Kulingana na mtandao wa PageSix, mwigizaji huyo ameanza kuandaa kazi yake mpya imayoitwa "Jumanji" akishirikiana na mastaa wengine Dwayne "The Rock" Johnson, Danny DeVito na Danny Glover.

Imeelezwa msanii huyo yupo vizuri kiafya, anatarajia kukamilisha kazi hiyo hivi karibuni baada ya kuahirisha huko nyuma kutokana na kukabiliwa na maumivu makali.





## Rihanna tambua kwenye raha kuna karaha

KILA kwenye raha kuna karaha! Ndivyo mwanamuziki Rihanna alipojikuta akipata kigugumizi baada ya kuulizwa swali lenye utata akiwa anajiandaa kulipamba jarida maarufu la Vogue.

Rihanna ambae alikaa kwenye kikaango na mtangazaji Anna Wintour, alimuuliza lini anatarajia kuwa na mtoto, ikiwa umri wake unasonga mbele.

Swali hilo lilimfanya mrembo huyo kupata kigugumizi cha muda lakini hakutoa jibu sahihi. Jarida hilo la Vogue litatoka mwezi Novemba.

## Studio ya Perry kufuru tupu

MASTAA mbalimbali wiki hii walishiriki ufunguzi wa studio kubwa inayomilikiwa na mwigizaji Perry mjini Atlanta.

Studio hiyo inatajwa kuwa ndiyo kubwa kuliko zote nchini humo na inamfanya kuwa Mmarekani mweusi wa kwanza kumiliki studio za filamu.

Mastaa kama Oprah Winfrey, Samuel L. Jackson, Beyonce, Will Smith na wengine wengi walikuwa ndani ya nyumba.

Studio hiyo imegharimu kiasi cha dola milioni 250, sawa na bilioni 75.3 za Kitanzania. Dola milioni 30, sawa na bilioni 69 zikitumika kununua kiwanja hicho cha hekari 330.





Na John Juma
0716217615

## MIONZI YA SHERIA

# Waweza kukiri tuhuma polisi ukazikana kortini

WENGI wetu tunajikuta tuko mbele ya polisi, watu wenye hasira kali au polisi jamii, kama mtuhumiwa umefikia hatua hiyo unaweza kukiri makosa katika kituo cha polisi au viongozi wa serikali za mitaa. Lakini kosa hilo ukalikataa unapopandishwa kizimbani kujibu mashtaka. Unaweza na yanatokea.

Mtuhumiwa anaweza kukubali au kukiri kosa fulani katika ngazi ya awali iwe kituo cha polisi au serikali ya mtaa ama polisi jamii ambako uvunjifu wa sheria umefanyika, lakini baadaye kukana mashtaka akiwa kizimbani.

Mshitakiwa licha ya kukiri makosa yake mara baada ya kufikishwa mahakamani anakataa kuhusika na uhalifu unaotajwa.

Ni kawaida sana tena mara nyingi mahakama zinashuhudia mshtakiwa mara baada ya kuwekwa chini ya ulinzi wa polisi au hata wananchi wenye hasira kali hujikuta analazimika au analazimishwa kukiri kosa.

Anafanya hivyo kwa kutegemea huruma au ahuweni fulani, hata kama hakufanya kosa analoshutumiwa nalo.

Zaidi sana, lengo ni kunusuru maisha yake kwa wakati huo.

Na kama haitoshi, wengine hufikia kukiri makosa hata kama hawajafanya kosa mara baada ya kuwa wameshapigwa sana wakati wa mahojiano katika mahabusu za polisi.

Hivyo basi, ni katika mazingira kama haya; mhusika hata awe jasiri kiasi gani anaweza kujikuta anakiri kosa ambalo kwa hakika hakukifanya na kupelekea kukataa kufanya hivyo mahakamani.

**ANGALIZO**

Ieleweke kuwa siyo jambo au atua nzuri sana mhusika kukiri kweli ametenda kosa, ili hali hajafanya hivyo itokee tu katika mazingira magumu, bila ya namna nyingine kuepuka mateso au mauti ikiwezekana.

Hii Kimsingi, wakati mwingine unaweza ukawepo ugumu wa kujinasua huko mbeleni, ukifikishwa mahakamani.

Mfano, katika kesi ya jinai namba 6/2017 kati ya Jamhuri dhidi ya Muhangwa Simon Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba chini ya Jaji I.C. Mugeta. iliyotolewa maamuzi hivi karibuni Septemba 25, 2019. Haya yalijiri.

Mshtakiwa alikiri kufanya mauaji hayo akiwa mbele ya polisi huko Biharamulo, na tena mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo huko Biharamulo. Ila mara baada ya kufikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama Kuu mjini Bukoba kwa ajili ya kusikilizwa kesi yake, akakamatwa akakataa .

Kabla ya kwenda mbali katika mazingira kama haya mahakama mara zote katika kuhakikisha haki inatendeka hujielekeza zaidi katika misingi mikuu mitatu ambayo hutakiwa kuthibitishwa na upande wa mashitaka ili kuonyesha kuwa mtuhumiwa ameamua kubadilika lakini alikiri.

Aidha, ieleweke kuwa upande wa mashitaka ndiyo wenye wajibu wa kuitosheleza mahakama kupitia misingi hii kuwa mtuhumiwa alikiri japo sasa anakataa kuwa hakukiri.

Kwa misingi hii ikiwa itatokea ukalazimika kukiri na baadaye kukataa, uweze kujua wanaokushitaki wanatakiwa kuthibitisha nini, au wewe uwahoji uwaulize nini na katika minajili ipi?.

Ambapo basi misingi yenyewe ni kama hivi , mosi wanaokushitaki wawe na ushahidi mwingine unaojitegemea unaoonyesha kuwa kweli umetenda kosa (collaboration).

Wasitegemee ushahidi huu wa kukiri pekee kwasababu huo tayari umeshaukataa.

Watafute ushahidi mwingine wa kuusaidia huu kuonyesha kuwa hata kama umekataa kuwa ulikiri bado kuna hili na lile linakuingiza kwenye kutenda kosa.

Ni wajibu wako kuwahoji kuhusu uwepo wa ushahidi mwingine tofauti na huu wa kukiri.

Wakikosa basi kukiri kwako kunakosa nguvu na hivyo kuleta uwezekano wa kuachiwa huru.

Pili, wanaokushitaki wathibitishe kuwa ulikiri bila kulazimishwa. Hii ni kwasababu kukiri kwa kulazimisha au kushawishiwa ni sawa na kuwa hujakiri au hukukiri. Wathibitishe kuwa hakukuwa na kulazimishwa. Hapa pia na wewe unayo kazi ya kufanya.

Kazi yenyewe ni kujitahidi kuonyesha mazingira ya kulazimishwa kukiri mfano alama za kipigo na mateso mwilini mwako, au mazingira ya hatari kama kuzingirwa na wananchi wenye hasira, au kundi na mazingira mengine yanayofanana na hayo. Ukifanikiwa katika hili basi umefanikiwa kufuta kukiri kwako na umekaribia kuachiwa huru.


Tatu, wanaokushitaki wathibitishe kuwa ulichokiri ulikuwa ukimaanisha hicho na si vinginevyo. Kwa maana kuwa kukiri kwako hakukulenga kitu kingine chochote bali lile kosa uliloshitakiwa nalo. Hii ni kwasababu waweza kuwa ulikiri lakini hukuwa umeelewa kile unachokiri.

Ni kazi yao wanaokushitaki kuthibitisha kuwa ulichokiri ulilenga kosa husika, lakini pia ni wajibu wako kama ulikiri bila kuelewa kuonyesha kuwa hukuwa umeelewa unakiri nini au mazingira hayakuwa rafiki kukupa nafasi ya kuelewa ulichokuwa unakiri.

Kwa ujumla wakishindwa kuthibitisha lolote katika haya matatu niliyoeleza basi ni shaka la msingi katika ushahidi wao hata kama ulikuwa umekiri yafaa mahakama ikubaliane na wewe kuwa hukukiri na uachiliwe huru.

Mwisho, kukiri kunakozungumziwa na makala hii kunajumuisha maelezo unayoandika polisi (cautioned statement) na yale yote unayoandika au kusaini popote nje ya mahakama kabla kesi yako kuanza (extra judicial statement).

Hivi ndivyo sheria inavyotaka.



Na Reubeni Lumbagala

## KALAMU YA MWALIMU

# Sera elimu bila malipo inavyoongeza wasomi

SERIKALI ya awamu ya tano imetimiza mwaka wa nne tangu iingie madarakani mwaka 2015. Mafanikio mengi yameonekana katika kipindi cha uongozi wa Rais John Magufuli, katika njanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Sekta ya elimu ni nyeti na ambayo katika miaka minne imepata mafanikio makubwa hasa kwenye utekelezaji wa Sera ya Elimumsingi Bila Malipo.

Elimumsingi Bila Malipo ni sera inayolenga kuhakikisha watoto wa Tanzania wanapata haki yao ya msingi ya kusoma bila kikwazo chochote na serikali kuu imebeba dhamana ya kugharamia elimu kuanzia ya awali hadi kidato cha nne.

Kupitia utekelezaji wa sera hii, wazazi na walezi wameachiwa jukumu la kuwapatia mahitaji muhimu watoto wao huku serikali ikituma fedha kila mwezi moja kwa moja katika akaunti za shule ili kufanikisha shughuli na mipango ya shule kama utawala, taaluma, mitihani, michezo na vifaa.

Kila mwezi serikali hutumia Sh.bilioni 24 katika utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Malipo, iliyoanza rasmi kutekelezwa Januari, 2016.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, anasema katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Magufuli, zimeshatumika takribani Sh. bilioni 934 katika utekelezaji wa jukumu hilo.

Kauli hii inaitoa alipokuwa akifunga mkutano mkuu wa kwanza wa wenyeviti wa walimu wakuu shule za msingi nchini hapa jijini Dodoma.

Waziri Nasha anasema "Kwa miaka minne sasa serikali inatekeleza mpango wa elimu bila malipo ambapo Sh. bilioni 24 zinatolewa kwa mwezi hivyo bilioni 943 zimeshatumika tangu serikali iingie madarakani".

Ni ukweli pasi na shaka kuwa sera ya Elimumsingi Bila Malipo imechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa hasa katika shule za msingi na sekondari nchini. Kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa sera hii, wazazi na walezi walikuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya kugharamia elimu ya watoto wao, jambo ambalo lilikuwa linachangia baadhi yao kushindwa kupeleka watoto wao shule kwa kuhofia gharama za kusomesha.

Kuanza kwa utekelezaji wa sera hiyo imekuwa mkombozi mkubwa kwa wazazi na walezi wengi ambao sasa hawana hofu ya kuwaandikisha watoto wao shuleni, kwani gharama za kusomesha watoto zinabebwa na serikali moja kwa moja.

Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza pamoja na kidato cha kwanza imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na mwamko wa wazazi kuwapeleka watoto wao shule na pia kuwahimiza watoto wao kujisomea kutokana na elimu kutolewa bila malipo.

Ongezeko la wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi na sekondari linachangia moja kwa moja kuongezeka kwa wasomi nchini katika miaka ijayo. Ili wasomi wapatikane ni lazima waanze kusoma elimu ya msingi, sekondari hadi vyuo vikuu. Hivyo basi, kutokana na kasi kubwa ya uandikishaji wa wanafunzi na idadi kubwa ya wanaojiunga na elimu ya msingi na sekondari, inachangia pia ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

Dira ya maendeleo ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hili haliwezi kutimia kama hakutakuwa na mpango mkakati wa kusomesha vijana wengi wa Tanzania ili kuja kutumika moja kwa moja katika shughuli za kiuchumi za kujenga nchi.

Kwahiyo, utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Malipo ni njia mojawapo ya kupata rasilimaliwatu yenye uwezo wa kutosha kutumika katika ujenzi wa nchi kwa kuchangia maarifa, stadi na ujuzi mbalimbali waliopata katika taasisi mbalimbali za elimu hapa nchini.

Sambamba na serikali kutumia bilioni 943 katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano, lakini pia serikali imetumia bilioni 308 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa shule za msingi na sekondari.

Uboreshaji na ujenzi wa mindombinu ya elimu hapa nchini imesaidia katika ongezeko la madarasa, mabweni, mabwalo, jambo linalochagiza kwa kiwango kikubwa ongezeko la wanafunzi shuleni.

"Kuanzia mwaka 2016 hadi sasa zimetumika Sh. bilioni 308 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa shule za sekondari na msingi," anasisitiza Ole Nasha.

Tunapoadhimisha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano, kama taifa hatuna budi kuunga mkono utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Malipo.

Pia, wazazi na walezi wawe tayari kushiriki katika kuwapatia mahitaji watoto wao ili waweze kusoma katika mazingira bora na hatimaye kukuza taaluma na kupata wasomi bora. Tutafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: (+255) 764 666349.**

# Kimiti amwona JPM kama Nyerere

Na Joseph Mwendapole

OKTOBA 14 mwaka huu, Watanzania wanaadhimisha kumbukumbu ya miaka 20 tangu kutokea kifo cha muasisi wa taifa hili, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyefariki dunia Oktoba 14, 1999 katika hospitali ya Mtakatifu Thomas, kule London Uingereza.

Mwalimu Nyerere, licha ya kustaafu urais mwaka 1985 na kufariki miaka 20 iliyopita, bado ameendelea kuishi katika mioyo ya wengi, wakikumbuka kwa uzalendo wake, ubinadamu na hasa kwa kujitolea na kuipenda nchi yake kwa dhati.

Ndiyo maana, kila mwaka, kila kona ya nchi, makundi mbalimbali, wakiwemo wasomi, wanasiasa, watafiti na wadau wa mambo mbalimbali, wamekuwa wakiendesha semina, makongamano, mijadala na tafiti mbalimbali zinazomhusu muasisi huyo wa taifa.

Mwaka huu, ukiwa ni wa nne tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, makongamano, midahalo na semina mbalimbali zimekuwa zikiendelea kuhusu kumbukuzi hii muhimu ambayo itafikia kilele chake Jumatatu ijayo ambayo kwa heshima yake, imepewa hadhi ya kuwa siku ya mapumziko kitaifa.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafuasi wa Mwalimu Julius Nyerere, unaohusisha wanasiasa mbalimbali waliofanya kazi karibu na Baba wa Taifa, Paul Kimiti, anazungumza na Nipashe kuhusu mambo mbalimbali kuelekea kumbukizi hii, akichambua ndoto za Mwalimu zinavyoakisiwa kwenye kazi za Rais John Magufuli.



Kimiti (kulia) akiwa kwenye maonyesho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO.**

## MAONO YANAVYOAKISIWA

Mzee Kimiti, ambaye enzi za Mwalimu alikuwa mwalimu wa siasa makao makuu ya chama, mkuu wa mikoa kadhaa na baadaye waziri, anazungumzia jinsi ambavyo ndoto ya kujitegemea ya Mwalimu Nyerere, inavyoshughulikiwa kwa kasi na weledi na Rais Magufuli.

"Sisi ambao tulifanya kazi kwa karibu na Mwalimu wakati wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, tunafahamu nini hasa ilikuwa ndoto yake. Mwalimu aliamini kwamba siyo jambo jepesi kwa nchi changa kama Tanzania wakati huo kuweza kuamua kufuata aina moja ya siasa ikiwa tegemezi, ndiyo maana akaanzisha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, akiamini kuwa kama taifa litajitegemea, kwa mahitaji yake yote muhimu, ni rahisi kuamua aina ya siasa ya kuifuata.

"Mwalimu alipenda sana taifa lijitegemee, lisiwe ombaomba kwa sababu siku zote ukiwa unaomba huwezi kuwa huru, ni lazima utafuata matakwa ya anayekupa kile unachokiomba.

Angalia, katika wakati ambao taifa lilikuwa limejitoa kuzisaidia nchi zingine za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara zipate uhuru wake, lakini bado aliweza kujenga viwanda vya bidhaa mbalimbali karibu kila mkoa, nia yake kuu ikiwa ni kujitegemea." Anasema Kimiti.

Anakumbusha zaidia kuwa :"Ukiangalia kwa umakini dhana hii, japo Mwalimu alishindwa kuitimiza wakati wa uongozi wake, lakini ni wazi kuwa Rais John Magufuli anaelekea kuitekeleza kwa kwa namna anavyofanya kila njia kuhakikisha kuwa taifa linajikomboa kutoka utegemezi wa mataifa ya nje na kuijengea uwezo wa kuweza kufanya mambo yake yenyewe," anaongeza.

## KAZI ZA NYERERE

Kimiti ambaye ndiye aliyesimamia shughuli zote za mazishi ya Mwalimu Nyerere, yaliyofanyika kijijini kwake, Butiama mkoani Mara, anasema anamtazama Rais Magufuli kama kiongozi ambaye ameamua kwa makusudi kuhakikisha taifa linajitegemea kupitia rasilimali zake.

"Mambo anayoyafanya hivi sasa yasingewezekana kwa kutegemea fedha za misaada. Siku zote watu wanaotukopesha hawapendi tujitegemee, wanatupa msaada wa leo ili kesho turudi tena kuwaomba na hivyo kuerndelea kuwa tegemezi." Anaongeza Kimiti.

Anataja mfano wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere Rufiji, akieleza kuwa mradi huo ukikamilika, taifa litakuwa limepiga hatua kubwa sana kuelekea kujitegemea, kwa sababu viwanda vingi vitakuwa na uhakika wa umeme kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimnbali.

"Ujenzi wa reli ya kisasa ya kutumia umeme, maana yake taifa litaweza kusafirisha abiria na bidhaa kwa wingi ndani ya muda mfupi, na hivyo kuharakisha maendeleo ya taifa kwa watu kuwa huru kupeleka bidhaa kokote wanakotaka kwa wakati.

"Wahisani siku zote wanataka tuwaabudu kwa kila jambo, angalia jinsi serikali ya awamu ya tano inavyofanya jitihada za kujenga vituo vya afya, hospitali kubwa na vifaa tiba nchi nzima. Hii inaondoa hofu ya kuwa na taifa ambalo haliwezi kuwapa tiba raia wake na hivyo kutegemea huduma hizo kutoka nje.

"Jambo la kufurahisha sasa ni kuwa vitu vyote hivi vinafanyika kwa kutumia fedha za ndani, kama ambavyo Mwalimu Nyerere alidhamiria. Serikali imedhibiti mianya yote ya rasilimali kuchotwa na watu wachache kwa faida yao, leo hii kodi inayokusanywa, mapato yanayopatikana kupitia rasilimali zetu mbalimbali, zinaonekana kwa sababu kila mmoja ni shahidi wa namna ambavyo taifa letu linasonga mbele.

"Mwalimu hakuruhusu madini kuchimbwa, kwa sababu aliamini wananchi wake hawajaelimika, akatoa fursa ya wanafunzi wote kusoma bure kwa gharama za serikali kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu, lengo lake lilikuwa ni kuzalisha wasomi ambao kwa elimu yao, wataweza kusimamia rasilimali za nchi kwa faida ya wote, " anasema.

Aidha, Mzee Kimiti anasema ujenzi wa reli, bwawa la umeme, hospitali na vituo vya afya vinavyoendelea kujengwa sehemu mbalimbali, vitaifanya Tanzania kuwa taifa la mfano miaka michache ijayo, kwani maendeleo, ni namna ambavyo wananchi wananufaika na huduma zinazotolewa, akitumia msemo usemao "Matajiri wote duniani hawafanyi kazi kwa ajili ya fedha bali wanafanya fedha ifanye kazi kwa ajili yao".

"Maana ya msemo huu ni kwamba ili tuweze kujua thamani ya fedha zetu, ni lazima fedha hizi ziwasaidie wananchi kwa kupata kwa uhakika na kwa wakati kwa huduma zote muhimu ikiwemo elimu, afya na nyinginezo," anasema Mzee Kimiti na kuongeza kuwa huo ndiyo msingi wa Ilani za Chama Cha Mapinduzi, kama mwongozo wa 1971, Ibara ya 28 inavyotamka kwamba "Kitendo chochote kinachompa mtu uwezo wa kuamua maisha yake na kutawala maisha yake, ni kitendo cha maendeleo, hata kama hakimwongezei afya wala shibe, lakini ni kitendo anachoamua mwenyewe".

Mzee Kimiti anaongeza : "Sera ambazo Mwalimu Nyerere alizikazania sana ilikuwa , ajira, mishahara na bei za bidhaa. Katika bei, aliamini kwenye ujamaa wa kweli, bei za vitu ni lazima zifanane, zisiwe na tofauti kubwa na hii ndiyo ilipelekea kuanzishwa kwa kampuni za biashara za mikoa maarufu kama RTC.

"Aidha Mwalimu hakutaka uwepo wa tofauti kubwa katika mishahara ya watumishi wa umma, hii ni kwa sababu kungekuwa na unyonge miongoni mwa wananchi, kama utaona, Rais Magufuli amepunguza sana mishahara ya watumishi kwa sababu mtu mmoja hawezi kulipwa milioni 40 kwa mwezi wakati mwingine anapata laki tatu.

"Utaona pia dhana ya Mwalimu ya uanzishwaji wa viwanda, alilenga kutoa ajira kwa Watanzania kwa sababu ndizo huchukua watu wengi, kitu ambacho Rais Magufuli anakifanya hivi sasa akihimiza ujenzi wa viwanda kila anapokwenda, akiamini taifa linakwenda katika uchumi wa kati na viwanda' anasema Kimiti.

# Aelezea Tasaf ilivyomtoa shimoni, anajihisi ‘bilionea’

**Na Elizabeth Zaya**

MWAKA 2014 ulianza kwa historia mpya katika maisha ya Editha Makala, mkazi wa mtaa wa Sokoine ulioko Singida Mjini, anayakumbuka haya, akisema: “Kama siyo Tasaf, sijui ningekuwa wapi leo, maisha yangu yalirudi nyuma nikafikia hatua ya kukata tamaa.”

Aidha, alianza kuona mwanga baada ya kikao cha wana mtaa wa Sokoine kumuidhinisha kuwa ni moja ya kaya maskini ili asaidiwe na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Mnufaika huyu na mama wa watoto watano,anahisi ulikuwa kama muujiza kwake baada ya Tasaf kuanza kumpatia Sh. 36,000, akisimulia kuwa pamoja na kiasi hicho kuwa kidogo, aliamini kwamba endapo akijipanga kuachana na umaskini kwa kuweka akiba baada ya kutimiza mahitaji ya watoto, angefanyia mambo ya maana.

Akizungumza na Nipashe wakati wa ziara ya wanahabari iliyoandaliwa na Tasaf mkoani Singida, hivi karibuni anasema aliendelea kujiwekea akiba hadi kupata fedha ya kununua cherehani ya kushonea nguo.

Ilikuwa nafuu kwake kwa vile anasema alikuwa na ujuzi wa kushona hivyo alijiunga na wenzake wawili na kuanza kushona lakini pia wakifanya biashara ndogondogo za kuuza mboga stendi ya Singida mjini.

Mnufaika huyo anasema aliendelea kupokea ruzuku ya Tasaf na kuweka akiba ya Sh. 100,000 iliyomwezesha kuanzisha mradi wa kuuza maji kwa kuyatembeza mitaani.

**KUONGEZA MTAJI**

Editha anasema baada ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya masakini alijiunga kwenye vikundi vya kuweka na kukopa jambo lililomsaidia kupata wateja katika biashara zake ndogondogo na pia uhakika wa kukopa hadi Sh. 200,000.

“Kipindi chote nilikuwa napambana ili mume wangu ajiunge nami nikamshauri tufanye biashara ya maji akakubali. Nikakopa pesa nyingine Sh. 200,000 kwenye kikundi nikanunua toroli la kubebea maji na madumu 12 gharama yake ilikuwa 136,000 nikamkabidhi mume wangu akaanza biashara. Wakati huo nami nikabaki na akiba ya Sh.100,000 kwa ajili ya biashara nyingine ndogondogo.” Anaeleza mama huyu.

“Mwaka jana niliondoka kwenye kikundi tulichokuwa tunashona kwa umoja na sasa nashona mwenyewe nyumbani na ninapata wateja namshukuru Mungu. Nimekuwa mtu anayeheshimika katika jamii, Tasaf imeniheshimisha sana.” Anaongeza.

“Mwanangu mdogo Elizabeth yupo kidato cha nne naye ananufaika na Tasaf kupitia ruzuku ya msichana. Wa pili ni Beatrice huyu anafanyakazi huko Dar es Salaam, anatusaidia kwenye mambo mbalimbali mpaka sasa yupo huko jijini.



Editha akiwa kazini nyumbani kwake. Anashona mavazi mbalimbali kwa rika zote. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

“Mwanangu wa tatu anaitwa Emmanuel huyu alisomea udaktari anafanya kazi Hospitali ya Mirembe kitengo cha masuala ya VVU na Ukimwi na mwingine ni Peter alisoma Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa alihitimu shahada ya elimu sasa hivi yupo jeshini kule Ruvu.” Editha anasema wanae wameanza maisha hivi karibuni na wanamsaidia na anafurahi kwa vile haba na haba hujaza kibaba na kwamba Tasaf imechangia kuboresha maisha yake , akishirikiana na mume wake wanauza maji kwa siku, hawakosi Sh. 3,000.

Aidha kwenye ushonaji anapata fedha kiasi hivyo wana uhakika wa chakula, pa kulala tayari amenunua kiwanja maeneo ya Nung’una Singida ambacho amekilipia Sh. 1,000,000, kwa awamu mbili na kwamba bado anadaiwa Sh. 200,000. Anazosema akimalizia kulipa anaanza ujenzi

**USHAURI**

Mjasiriamali Editha anawashauri wengine wanaokumbwa na matatizo na changamoto za umaskini wasikate tamaa mapema bali wajenge tabia ya kupenda kuanza upya.

“Sijawahi kukata tamaa na sitafanya hivyo nawashauri wengine pia kufanyakazi kwa bidii hasa biashara ndogondogo wasizidharau, zinaongeza kipato ila cha muhimu ni kujiwekea malengo na kuwa na nidhamu na uvumilivu.

“Namshukuru Rais John Magufuli namuomba aiongezee nguvu Tasaf ili iendelee kuwakomboa wanyonge, tunajua kwamba yeye ni mtetezi wa wanyonge na hili tunaliona katika kazi zake.”

**HISTORIA**

Editha anakumbuka kuwa familia yake ilianza kuyumba baada ya mume wake kupata changamoto zilizomuondoa kazini katika moja ya kampuni za umma .

Kabla ya kupata tafrani hiyo maisha yao yalikuwa bora na walijenga nyumba ya vyumba 14 huko Singida mjini Mtaa wa, Majengo,ugumu wa maisha ukikolea zaidi mwaka 1999 na kulazimika kuuza baadhi ya mali zikiwamo samani ili kupata nauli ya kurudi nyumbani Singida kwani awali walikuwa wakiishi mkoani Tanga.

“Licha ya maisha magumu sikupenda watoto wangu wakose elimu nilihangaika kwa kukopa, kuomba misaada na biashara ndogo ndogo. Ilifika wakati nakosa hata hela ya panadol, kulala njaa ilikuwa jambo la kawaida kwangu, na hata watoto wangu walizoea,”anasema.


**NYUMBA KUNADIWA**

Kwa Editha kukimbiwa na ndugu si jambo geni, anasema aligundua kwamba dhiki ni kitu kibaya, kwa sababu ilifika kipindi hata ndugu, rafiki na jamaa zake wa karibu walikuwa wanamkimbia alipowaomba msaada

Anasema mwaka 2012 benki ilipiga mnada nyumba yao ambayo walikuwa wakiishi baada ya kushindwa kulipa deni walilokopa kwa ajili ya ujenzi, hivyo kulazimika kuanza kuhangaika kusaka makazi mtaani.

“Nyumba ilikuwa haijakamilika iliuzwa shilingi milioni 6.5 tukapewa Sh. 400,000 kwamba ndicho kilichobaki. Ilibidi hiyo iliyobaki ndiyo tuitumie kwenda kutafuta nyumba ya kupanga ili tuanze maisha mapya ya vyumba viwili hapa Sokoine,” anasema Editha. Anasema maisha yalizidi kuwa magumu lakini kwa msaada wa Tasaf maisha yake yamebadilika na sasa anaimba wimbo wa maendeleo siyo umaskini.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 15 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Makao makuu ya shirika la Afya duniani
3. Kipindi baina ya mawio na machweo
8. Nchi ambayo ni bara
10.Hakimu wa Kiisamu
11.Eleza 12. Fungua kamba ili zisikaze 16. Acha kufanya jambo 17. tarakimu
19. Vuta pumzi ili kuhisi harufu 22. Hutumika kusikia
24. Kiwango
25. Nchi inapoishia
26. Toa yai katika kiloaka
27. Keti 28. Kandanda, soka

**Dondoo: Chini**

1. Matumizi makubwa ya pesa
2. Ukoo 4. Fanya kuwa zee
5. Sujudia 6. Orodhesha
7. Sehemu ya kuingilia ndani
9. Pesa itumikayo Omani
13. Eka 14. Tunda la mwembe
15. Umbo
17. Wingi wa uwanda
18. Weka nafaka juani zikauke
19. Mwanamieleka Edward Fatu
21. Mno 23. Neno la kuomba
24. Mtaa

## Jibu Na: 14

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | L | G | E | R | I | A | | O | | A | | |
| S | | E | | | | | U | Z | U | R | I | |
| M | O | R | O | C | C | O | | W | | I | | K |
| A | | E | | | | | K | A | M | A | S | I |
| R | U | Z | U | K | U | | A | | | | | L |
| A | D | A | B | U | | A | M | A | Z | O | N | I |
| | H | | A | H | A | D | I | | | | | O |
| K | A | M | B | A | | H | A | K | I | M | U | |
| | M | P | E | N | Z | I | | E | | A | | T |
| N | I | A | | I | | B | | S | I | J | U | I |
| A | N | N | A | | S | I | S | I | M | I | Z | I |
| M | I | G | U | U | | W | | | B | | W | |
| I | | O | A | | Z | A | M | B | A | R | A | U |

SIKU YA BINTI DUNIANI

# Kutibu kiherehere 'curiosity' kutamaliza mimba utotoni

Na Gaudensia Mngumi

KILA mwaka Oktoba 11 ni siku ya kimataifa ya mtoto wa kike duniani. Tanzania inaadhimisha siku hii wakati kukiwa na ongezeko la mimba za utotoni na wiki hii Rais John Magufuli, anahoji, inakuwaje taifa lina polisi, mahakama, sheria, wabunge, wakuu wa mikoa, vijiji na kata lakini hakuna wa kuwalinda wasichana?

Akiwa mkoani Rukwa na Katavi anawauliza Watanzania inakuwaje wasichana 299 wamepata mimba Rukwa kwa mwaka mmoja lakini hakuna idadi kama hiyo ya wanaume wanaotumikia kifungo cha makosa ya ubakaji mabinti.

Anasema ni jambo linalolitia doa taifa hivyo viongozi watumie vyombo na taasisi za dola kutokomeza mimba za utotoni ili wasichana wasome kwa kuwa serikali inagharamia elimu kwa kutoa mabilioni kila mwezi, hivyo kila mmoja asome na wasichana wasiachwe nyuma.

Pamoja na agizo la Rais ni wakati wa wazazi, walezi, waalimu na wadau wa elimu na malezi kutafakari sababu za mabinti kupata mimba na kuzitafutia ufumbuzi, si vyema janga hili kuendelea kukosa ufumbuzi kwanza kwa kuangalia 'kiherehere.'

Akiwa katika ziara za Rukwa na Katavi, Rais anawaasa mabinti kuacha 'kiherehere' na kutulia kwani watakuwa mama na kupata watoto wakati ukifika.




Kuwasomesha mabinti ni muhimu kwani wasichana wa chini ya miaka 18 wakipewa mimba na kuwa wamama kwenye umri mdogo ni kupalilia umaskini. Kwa hiyo kuwalinda na kuwatetea mabinti kusichukuliwe kama 'kelele za chura' bali kama jukumu la kila Mtanzani ili kuwa na taifa lenye watu walioelimika. PICHA: MTANDAO. **PICHA: MTANDAO**

### DAWA YA KIHEREHERE

Mabinti kama binadamu wengine wanakuwa na kiherehere au 'curiosity'. Kwa kuwa hoja ni huo mhemko wazazi, walezi na walimu shuleni pamoja na wadau wa elimu wanatakiwa kuwasaidia mabinti kukabiliana na mhemko huo.

Kama walivyo wanaume mabinti nao husikia taarifa nyingi kuhusu kujamiiana, kuwa na marafiki wa kiume na mambo mengi yanayoeleza uzuri wa ngono.

Ndiyo maana nao wanahisi kuwa 'hebu nijaribu', 'hebu nifanye nijue kuna nini kwenye kujamiiana'.

Iwapo walezi au walimu na wadau watawaeleza watoto kuhusu ngono na wakafahamu kwa kina kuwaza huko hakutawaathiri kwa vile kiherehere kitakuwa kimedhibitiwa kwa kuelezwa athari na faida za ngono utotoni.

Kwa hiyo, huenda kuwaeleza mabinti masuala ya ngono na kuwafundisha kikamilifu, matokeo mabaya kama vile kupata maradhi hasa VVU na Ukimwi, ujauzito, utoaji mimba usio salama, kuacha shule na kuwa mama wakingali watoto yote haya yatapunguza kiherehere.

Mabinti yafaa wafundishwe hatua kwa hatua masuala ya kujamiiana kuanzia madarasa ya chini hadi wanapofikia kidato cha sita ili waelewe na kufahamu ukweli badala ya kuishi na kuongozwa na 'curiosity' au kiherehere hicho.

### KUTOJUA UKWELI

Kukosa ufahamu juu ya ukweli wa masuala ya kujamiiana ni jambo linalochangia kupata mimba za utotoni. Moja kwa moja lawama hapa zinawaendea wazazi . Ni wengi ambao zama hizi hawazungumzi na watoto wao kuhusu ngono na kuamini kuwa walimu shuleni na dunia zitafanya kazi hiyo.

Walezi na wazazi wakumbuke kuwa walimu hawana nafasi. Wana kazi nyingi wakati mwingine ni wachache shuleni na hawawezi kufanya kazi zote ikiwamo kuwaeleza mabinti kuhusu michezo na athari za kujamiiana.

Ni wazi kuwa watoto wengi hawashauriwi wala hawaelezwi ukweli kikamilifu kuhusu kujamiiana, ndiyo maana mabinti hata wa kidato cha sita wanaweza kuwa na mimba lakini hawafahamu kuwa ni wajawazito.

Mathalani, mabinti wanaambiwa ukifanya 'ngono mara moja hupati mimba'. Wanadanganywa pia kuwa kwa kutumia 'staili' flani hawatapata ujauzito. Si hivyo. Wengi hawajui kuhusu mzunguko wa hedhi na siku za kupata ujauzito ama nyakati ambazo watapata ujauzito.

### UJINGA

Mabinti wengi ni wajinga kutokana na umri wao hivyo , wavulana au wanaume hutumia udhaifu huo na kuwapa ujauzito. Wapo wanaopata mimba wakienda au kurudi nyumbani kutokana na kucheza na wanaume njiani. Wengine huwapeleka vichani au porini. Hupata mimba kwa vile hawajajua kuwa kucheza na wanaume kwenye umri huo wa kupevuka ni hatari.

Ujinga husababisha mabinti kushindwa kusema hapana, au sitaki kufanya ngono pale kijana au mvulana au mwanafunzi mwenzake anapomtaka kufanya hivyo. Wakati mwingine msichana na anadhani kuwa kukataa kutasababisha aonekane mshamba kumbe sivyo. Ndiyo maana hapa cha msingi ni wazazi, walimu, walezi na wadau wakereketwa wa haki za watoto wasichoke kuwaeleza wasichana athari za kufanya ngono utotoni.

### MAISHA DUNI

Watoto wengi hushika mimba kutokana na maisha duni nyumbani kwao. Kwa mfano hawana faragha. Huchangia chumba kimoja watoto wa kike na wa kiume na hata ndugu wa kiume. Wakati mwingine wageni huwafundisha wasichana hawa tabia mbaya na kuwabaka na kupata mimba zisizotarajiwa.

Umaskini huo wa kipato unaoleta makazi duni, ukosefu wa chakula na mahitaji muhimu ndiyo unaosababisha mimba kwa mabinti. Wanaume wengine wakiwamo madereva wa kuanzia pikipiki , daladala na hata malori pia wajasiriamali huchukulia udhaifu huo na kuwadhalilisha kingono.

Wakati mwingine hutumia kigezo hicho kuwa binti au msichana flani ni maskini ukimpa fedha kidogo , au kanga, chakula na pengine lifti kwenda na kurudi shuleni umempata. Hufanya hivyo hatimaye binti kupata ujauzito na kulazimika kuacha masomo akizaa mtoto ambaye hamfahamu baba yake wala hawezi kumbana mhusika kwa vile alikuwa akijamiiana na watu wengi.

Ndiyo maana kama Rais alivyosema ni lazima sheria, polisi, viongozi, wazazi na walezi wanawajibika kuwalinda watoto popote iwe njiani, kwenye bodaboda na kuhakikisha 'mafataki' na wote wanaohujumu wasichana wanajulikana na kuchukuliwa hatua tangu mwanzo kwa kukamatwa na kufikishwa mbele ya sheria.

Ni ukweli kuwa mimba za utotoni wakati mwingine zinatokana na walimu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wasichana iwe shule za msingi hadi sekondari.

Wasichana wanabakwa na walimu wao iwe ofisini, nyumbani kwa walimu, wengine mashambani, porini au hata kwenye nyumba za wageni.

Watanzania wanapenda kuchunguza mwenendo wa walimu kuanzia mavazi, ulevi, kiwango cha maisha na pale anapokosea hunyooshewa kidole kuwa mwalimu flani ni mchafu, mlevi au anaishi maisha ya dhiki. Hata hivyo hakuna anayeweza kumnyooshea kidole anapowaharibu mabinti. Jamii sasa ipambane na udhaifu huo na kuwakanya walimu hao. Hata Tume ya Walimu ihusike, maofisa elimu na kamati za shule zisiwaogope kwani walimu kwa walimu hulindana.

### USHAURI NASAHA

Ili kuondoa mimba shuleni, shule zinahitaji washauri nasaha wawe walimu, wadau wa saikolojia na wataalamu wa fani hiyo, kuwafundisha watoto masuala ya ngono, kupevuka, uzazi, mimba utotoni, utoaji mimba usio salama na utoro.

Inawezekana wasichana wakafundishwa na kuelezwa masuala haya kama serikali itagharamia mafunzo ya ushauri nasaha kwa walimu na wadau wengine kutoka asasi za kiraia wakaunga mkono kwa kutoa mafunzo.

Taasisi za dini nazo zina mchango. Kwa pamoja wadau hao na walimu wakiwafundisha mabinti kuwa kupitia 'kiherehere' watapata watoto wakiwa na umri wa utoto, kiherehere kitawasababishia kufukuzwa shuleni, kuambukizwa maradhi ya VVU na Ukimwi na pia kinaweza kusababisha hata kupoteza maisha kwa kujifungua kwenye umri mdogo na hasara nyingine nyingi, tatizo linaweza kupunguzwa.

## HABARI KIMATAIFA

# Kitanzi adhabu wapenzi jinsia moja Uganda

**KAMPALA,** Uganda

UGANDA imefanya mabadiliko ya sheria kuruhusu kunyonga wapenzi wa jinsia moja.

Waziri wa maadili nchini Uganda ametangaza mipango wa kuanzisha tena sheria inayopinga mahusiano ya jinsia moja, iliyofutwa na mahakama ya kikatiba mwaka 2014.

Waziri Simon Lokodo, aliliambia shirika la habari la Reuters kuwa sheria hiyo mpya itamuadhibu hukumu ya kifo yeyote atakayeenda kinyume nayo.

**Tunajua kuwa kitendo hiki kitawachukiza watu wengi wanaotusaidia kwenye uongozi na masuala ya bajeti lakini...**

"Sheria yetu ya sasa inatubana sana. Inasema kuwa kitendo hiki ni jambo la kuvunja sheria. Tunataka iwekwe wazi kuwa mtu yeyote anayepigia debe suala hili anaweza kushtakiwa. Wale wanaofanya vitendo vya kushangaza watahukumiwa kifo."

Aliendelea kueleza kuwa, "mahusiano ya aina hii sio kitu cha kawaida kwa watu wa Uganda na kumekuwa na waajiriwa wengi shuleni ambao ni wapenzi wa jinsia moja wanaowafundisha watu uongo kuwa mtu anazaliwa na hisia za mapenzi ya jinsia moja."

Mwezi Februari mwaka 2014, Rais Yoweri Museveni, alisaini muswada wa sheria wa kuwabana wapenzi wa jinsia moja lakini sheria hiyo ilifutwa na mahakama mwezi Agosti mwaka huo huo.

Mabadiliko hayo yalitokea baada ya kubainika kuwa wabunge walipitisha sheria hiyo bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Waziri Lokodo alisema muswada mpya ambao utawasilishwa bungeni wiki zijazo unaungwa mkono na wabunge pamoja na Rais Museveni.

Tumekuwa tukizungumza na wabunge na tumehamasisha idadi kubwa, wengi wao wanakikubaliana na jambo hili."

Miaka mitano iliyopita nchi za Afrika Mashariki waliwekewa vikwazo na Marekani kwenye uombaji wa viza na wakasitisha utoaji msaada na mazoezi ya kijeshi, hata hivyo Lokodo alisema kuwa nchi yake ipo tayari kwa mashambulio yoyote watakayoyapata juu ya kampeni hiyo.

"Hatupendi kutumiwa'," alisema waziri huyo.

"Tunajua kuwa kitendo hiki kitawachukiza watu wengi wanaotusaidia kwenye uongozi na masuala ya bajeti lakini..." **BBC**



Moja ya shule ya miundombinu mibovu iliyofungwa. **PICHA: DW**

## Shule zafungwa zakosa majengo

**MOMBASA,** Kenya

AGIZO la Wizara ya Elimu nchini Kenya kufunga shule zote zilizo na majengo yasiyokuwa imara, limekwamisha shughuli za elimu katika shule za badala kwenye vitongoji duni na kutatiza masomo ya watahiniwa wa darasa la nane.

Shule hizo zinazofahamika kama APBET, zinatoa elimu katika mitaa ya kimasikini ya makazi maskini ya banda katika miji mikuu ya Mombasa, Nairobi, Kisumu na sehemu zilizo na ukame nchini Kenya. Mjini Mombasa shule 14 zimefungwa hivyo kukwamisha masomo ya watahiniwa takribani 36. Moja ya shule zilizofungwa ni shule ya msingi ya Agatha iliyoko katika mtaa wa Bangladesh. Shule hiyo imefungwa kwa sababu ya kujengwa kwa mabati na kukosa miundombinu bora.

Kupitia kanuni ya mwaka 2009, serikali ya Kenya inazitambua shule hizo za kibinafsi za mbadala ambazo aghalabu zimejengwa kwa mabati au mbao na kukosa miundombinu bora kulingana na kanuni za elimu, hata hivyo wizara hiyo ya elimu haikuzizingatia wakati ikitoa agizo la shule zisizokuwa na majengo bora kufungwa.

Wanafunzi wengi walikuwa wanasoma katika shule za majengo hatari. **DW.**

# Waziri Mkuu Ethiopia mshindi Nobel

**OSLO,** Norway

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ameshinda tuzo ya amani ya Nobel kwa mwaka 2019 na ametunukiwa tuzo hiyo kwa kutambua jitihada zake za kuleta amani na ushirikiano wa kimataifa.

Mkataba wa amani ulisainiwa mwaka jana, mgogoro wa kivita na nchi jirani uliochukua karibu miaka 20 tangu mwaka 1998-2000, alishiriki kuumaliza na kuutatua kwa maendeleo ya nchi yake.

Ahmed (pichani) alitajwa kuwa mshindi wa 100 wa Tuzo ya Nobel Peace Prize huko Oslo.

Jumla ya washiriki 301 waliochaguliwa katika tuzo hizo zenye hadhi kubwa duniani, washiriki 223 ni watu binafsi na kampuni 78 .

Tayari watu walikuwa wamekisia nani angeshinda tuzo. Chini ya kanuni za asasi ya Nobel, washiriki waliotajwa majina yao hayaruhusiwi kuchapishwa hadi ipite miaka 50.

Mwanasayansi wa Sweden, Alfred Nobel alianzisha kwa mapenzi yake tuzo hizi mwaka 1895, aidha hutolewa tuzo tano kwenye fani za kemia, fasihi andishi, tuzo ya amani, fizikia na fiziolojia ambayo ni elimu ya dawa.

Baada ya Ahmed kuwa Waziri Mkuu Aprili, 2018, alianzisha mabadiliko Ethiopia akiwaachia huru maelfu ya wanaharakati waliokuwa gerezani na wale walio uhamishoni kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Jambo la muhimu zaidi Waziri Mkuu huyu alilofanya ni kusaini mkataba wa Amani na nchi jirani ya Eritrea kumaliza mgogoro baina yao ambao ulichukua miongo miwili.

Lakini mabadiliko au harakati alizozifanya zilipelekea nchi hiyo kutokuwa na utulivu na watu milioni 2.5 walilazimika kuhama makazi zao kutokana na vurugu.

Swali linaloulizwa ni kwa nini Abiy Ahmed alishinda? Kamati ya tuzo hiyo ya Nobel katika hutuba yake , ilisema kuwa ametunukiwa tuzo hiyo ya heshima kwa kufanikiwa kutatua mgogoro wa mipaka na nchi jirani ya Eritrea.



"Tuzo hiyo ina maana kuwa imetambua juhudi za washirika wanaotaka amani na makubaliano nchini Ethiopia, Afrika Mashariki na Afrika yote kwa ujumla," waandaji walisema katika taarifa yao.

Baadhi ya watu waliopata tuzo hiyo Rais wa zamani wa Marekani Barack Obama alishinda tuzo ya amani ya Nobel mwaka 2009, kwa jitihada za kuimarisha diplomasia ya kimataifa na ushirikiano baina ya watu.

Rais mwingine wa Marekani , Jimmy Carter mwaka 2002 wakati washindi kutoka Afrika ni pamoja na Denis Mukwege wa Congo, alishinda kwa juhudi zake kukabiliana na udhalilishaji wa kingono nchini humo.

Askofu Tutu, Desmond wa Afrika Kusini, alipata tuzo ya amani ya Nobel mwaka 1984 kwa kupinga na kukemea ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini .

Rais mstaafu wa Liberia Johnson Sirleaf, Ellen alipata tuzo ya Amani ya Nobel mwaka 2011 kutokana na juhudi za kupambania usalama wa wanawake , haki za wanawake na ushiriki wa wanawake katika kazi ya kuijenga amani ya Liberia. Mwanamama huyu ni rais wa kwanza mwanamke barani Afrika aliyechaguliwa kidemokrasia.

Profesa Wangari Maathai wa Kenya, alitunukiwa tuzo ya amani ya Nobel kwa jitihada zake katika kupigania haki za binadamu na haki za wanawake na utunzaji mazingira. **BBC**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 22

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




Na Adam Fungamwango

ILIMCHUKUA wiki nzima mama Kadili kuelewa somo. Aligundua ndani ya gazeti la Nipashe analopenda kuzurura nalo kijana wake kuna picha ya msichana aliyesababisha kutekwa na kupelekwa asikokujua kwa siku tatu.

Baada ya kijana wake kujisahau na kuacha gazeti, aliitazama picha hiyo ya Edina kuolewa na mwanaume tajiri.

"Haka ndiko kasichana kanakomsababisha kijana wangu matatizo?" Aliangalia kwa makini mwishoni akajisemea. "Mh! Kumbe kazuri. Kana haki. Ila kalitaka kumuua mwanangu, bora kalivyoolewa." Mama Kadili alikuwa akijisemea mwenyewe kimoyomoyo.

Nusu saa baadaye Kadili aliingia na kumkuta mama yake subuleni.

"Shikamoo mama."

"Marahaba Kadili, lakini nina mazungumo na wewe kidogo."

"Mimi mama."

"Ndiyo wewe sasa nani?"

"Haya." Aliitika na kukaa kwenye kochi."

"Enhee kiko wapi mwanangu." Alianza mama na maneno hayo yalimshtua Kadili.

"Nini kwani mama?"

"Nilikwambia nimekuzaa mwenyewe kwa hiyo ukiwa na furaha hata kama unaificha najua, na hata akiwa na huzuni ukiificha pia najua." Mpaka wakati huo Kadili hakutaka kuongea lolote, kwani alishajua kuna kitu ambacho mama yake ameshagundua kama kawaida yake.

"Nilikwambia mwanangu, yule msichana ni mtoto wa kitajiri huwezi kumpata, sasa ameolewa na wenye nazo.

Ndiyo maana wiki yote hii hujachangamka. Ameshaolewa, cha kufanya msahau huyo binti, masomo umeshamaliza na sasa umri wa kuoa tayari." Alimeza funda moja la mate akamwangalia kijana wake kwa makini.

"Wiki iliyopita nilikwenda Mtoni Mtongani kwa mjomba wako Polly. Katika maongezi tuliyoongea ni kwamba tumekubaliana wewe umuoe binti yake Eliza." Habari hiyo mpya ilimshtua Kadili. Anamfahamu Eliza. Ni ndugu yake. Ni mpwa wake. Binti ya mjomba wake aliyezaliwa na mama yake. Ni msichana mrembo na anafaa kuwa mke.

"Mbona Eliza ni mzuri tu, tena huyu ni mtu wetu wa karibu, hatokuumiza kijana wangu." Kadili hakupinga wala kukubali. Eliza ni msichana mrembo, anayekaribiana na Edina, lakini bado hajamfikia.

Edina alikuwa ni habari nyingine. Kadili hakutegemea kama mama yake anaweza kumwambia jambo kama hilo.

"Sawa mama nimesikia, sijakataa ila ni mapema mno, lakini hilo mlililoliamua si baya, ila linahitaji muda."

"Na wiki ijayo atakuja hapa, mwenyewe ameshakubali. Atakuja ili muongee wenyewe, maana sisi tumeshayamaliza."

Kulizuka ukimya wa dakika na ukamalizwa na Kadili mwenyewe.

"Haya." Alijibu.

**********************************

Miezi kadhaa ilipita. Eliza alikuwa akifika mara kwa mara nyumbani kwa kina Kadili. Alikuwa akizunguka naye mtaani. Kila mtu sasa alijua kuwa Kadili amepata mpenzi. Ni wachache sana waliojua kuwa ni mtoto wa mjomba wake. Kwa kiasi fulani Eliza alituliza mawazo ya Kadili kwa Edina.

Kama kawaida yake, siku moja aliamka na kwenda kando ya barabara ya Tandale, Sinza Magomeni, maeneo ya Tandale kwa Mtogole.

Ilikuwa ni kama ada, akakutana na kundi la watu ambao walikuwa akibishana soka. Mashabiki wa Simba walikuwa wakiwacheza wenzake wa Yanga kupangiwa na timu ya Misri, Pyramids kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Walikuwa wakiaambia kuwa hawatoki kwa sababu timu wanaoyokutana nayo, ingawa ni ndogo, lakini ni tishio.

Wenyewe mashabiki wa Yanga walikuwa wakipinga vikali kuwa hata iweje, waarabu safari hii hawatoki Taifa.

"Tunawamaliza hapa hapa, huko kwao tutaenda kukamilisha kazi tu." Alisikika mmoja wa mashabiki wa timu hiyo.

Kadili hakuwa mpenzi sana wa soka, lakini alipenda mno mabishano ya mashabiki, hasa wale waliokuwa wakishindana kwa hoja na si matusi, jazba na ugomvi. Alinunua gazeti la nipashe kama kawaida yake na kurejea nyumbani. Safari hii hakutaka kuremba. Alianza kulisoma kurasa moja baada ya nyingine kwa umakini. Alipofika kwenye ukurasa wa matangazo na matukio, alikutana na picha kubwa, pamoja na tangazo.

Ni picha ya mtu ambaye anamfahamu. Juu kulikuwa na maandishi makubwa. 'Amepotea.'

"Edina amepoteza? Ameenda wapi? Kwa nini?" Alijiuliza.

Picha ilikuwa ni ya Edina. Haikuwa ile ya miezi sita iliyopita ambayo ilikuwa ni ya harusi. Ilikuwa ni picha nyingine tofauti. Akaanza kusoma maelezo yaliyokuwa chini ya picha ile.

'Mwanamke mmoja, Edina Barton, amepotea baada ya kutoweka nyumbani kwa mumewe Dk. Fiston Kabanga.

Edina ana siku ya nne sasa tangu aondoke nyumbani hapo bila taarifa yoyote na mumewe amejaribu kumtafuta maeneo yote imeshindikana. Yoyote atakayemuona, basi awasiliane na mumewe, au kituo cha polisi kilicho karibu naye. Zawadi nono itatolewa."

Tangazo hilo lilimaliziwa na namba za simu za mume wa Edina.'

Vyovyote itakavyokuwa, lakini ukweli alioupata Kadili hapo ni kwamba Edina hayupo kwa mumewe kwa sasa.

"Kwa nini? Amepatwa na matatizo gani? Ametekwa na watu wasiojulikana? Amepata ajali na mwili wake umeshindwa kupatikana hadi leo? Au ametoroka mwenyewe?"

Hayo ni mawazo yaliyokuwa aliyokuwa nayo Kadili. "Na kwa nini atoroke wakati ndoa ameitaka mwenyewe na mama yake?" Alijiuliza mwenyewe na hakupata jibu.

Kengele ikagonga kwenye kichwa cha Kadili kuwa kwa hili lililotokea, basi huenda hata yeye lisimuache salama.

Kama Edina atakuwa ameuawa au kupata ajali, itakuwa ni simanzi kubwa kwa Kadili kwa sababu ni mwanamke ambaye alimkubali na kumuweka moyoni, licha ya kwamba hakuwahi kupata nafasi ya kumuelezea maswahibu yake ya moyoni. Utakuwa ni msiba mkubwa kwake.

Kama atakuwa ameamua kumtoroka mumewe, basi hata kama atakuwa amekwenda sehemu nyingine, lakini mtu wa kwanza kushukiwa anaweza kuwa ni yeye.

"Edina utaniponza tena Edina. Mama yako anaweza kudhani uko kwangu." Kadili alijikuta akilalamika peke yake.

Akili ilianza kumtuma kuwa kwa siku hizi mbili tatu, aondoke nyumbani kwao na kwenda kuishi sehemu nyingine kwa muda. Kwa siku hizi, nyumbani kwao utakuwa ni sehemu ya hatari, kwani watakapokuwa wakimsaka, moja ya sehemu ambayo inaweza eneo sahihi la kutafuta ni nyumbani kwao.

Kama mama yake aliweza kutuma mabaunsa na kufika kwao, wakamchuka na kumpeleka kwake, haitoshangaza sasa akaja na askari kuja kumsaka Edina, ambaye hawatomuona na baada ya hapo, akaweza kuchukuliwa yeye kwa ajili ya kuisaidia polisi, hadi hapo atakapopatikana akiwa hai au maiti yake.

Lakini pia ithibitike kuwa kupatikana kwake huku awe hai au amekufa, hakukuwa na uhusiano wote na yeye, hapo ndipo atakapokuwa huru.

Wazo lingine lilimjia Kadili. Kama akiondoka kwao kwa ajili ya kukimbia tatizo hili, wakija askari na kutomkuta, inaweza kutafsiriwa kuwa yupo pamoja na Edina huko aliko.

Yaani inawezekana ikaonekana ni yeye aliyemshawishi au kumsaidia kutoroka. Kwa vyovyote vile, katika hili aliona kuna kitu kinakuja mbele yake, hivyo inambidi awe makini.

Na moja ya tahadhari ni kuchagua ama aondoke nyumbani, au aendelee kukaa. Yote mawili aliyeona ni mazuri na mabaya pia. Mwisho akaona bora amshirikishe mtu katika hili. Ni nani? Akaamua jambo hili mama yake ndiyo aamue, hivyo ni lazima amwambie kwanza ajue nini kimetokea, ndiyo wajue nini la kufanya.

**Mwisho akaona bora amshirikishe mtu katika hili. Ni nani? Akaamua jambo hili mama yake ndiyo aamue, hivyo ni lazima amwambie kwanza ajue nini kimetokea, ndiyo wajue nini la kufanya.**

**Itaendelea Jumamosi**

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**SHAMBA LINAUZWA**, Hekari 25@ Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 76/2019**

AMOSI ISMAILI MTAKUBWA …………………..MDAI

DHIDI YA
1, MAGRET OSCAR
2,VEDASTUS RUGACHWA
3, OSCAR RUGACHWA
} ……… WADAIWA

KWA: MAGRET OSCAR NA OSCAR RUGACHWA.
(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 76/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 28.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 07.10.2019

115459502

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**FURAHA JOSEPH TEMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.427/0662 kilichotolewa na MAKAMBAKO SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/MPW/RB/373442/2019.

115459202

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 82 OF 2019
In the matter of the Estate of the late GODSON CHRISTOPHER SAILENI
And
In the matter of the Application for letters of Administration by REHEMA GODSON SEILENI

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the day of 01st/11/ 2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Date at Dodoma this 30th of September 2019

Petitioner
Presented for filling this 30/10/2019

RESIDENT MAGISTRATE

115458902

---

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**HERIETH JOEL KUSEKWA** anatangaza kupotelewa na CHETI CHA KIDATO CHA NNE CSEE NA. S.0256-0019 kilichotolewa na shule ya Sekondari Huruma Girls 2008 na Cheti Cha KIDATO CHA SITA ACSEE NA. S.578-0570 kilichotolewa na shule ya Sekondari Taqwa mwaka 2011. Vyeti vilipote Mwanza eneo la Nata.

Yeyote atakazïona atoe taaria polisi
MW/RB/8170/2015

115459102

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOYCE MBUYA LIFA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0784-0090/2015 kilichotolewa na AIRWING HIGH SCHOOL mwaka 2015.


Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/CEN/RB/363243/2019.

114458002

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**NDG.DORIKA MBOGELA**
Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha IV (Nne), ambacho kilitolewa na Baraza la mitihani Taifa kupitia shule ya sekondari ya Kinyala, chenye Index Na.S.0794/0008.

Kwa yeyote atakayekiona aripoti kituo cha polisi kilicho karibu.

TAARIFA YA POLISI:
MB/RB/490612014.

115458102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA: 63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya …………..MJINI …TANGA**
**Wilaya ya TANGA**

**MADAI NAMBARI…29….. ya…. 2019**

Mdai HARUNA HUSSENI MUSSA
Mdaiwa ALLY BAKARI

Kwa: ALLY BAKARI
C/O MWENYEKITI MWAHAKO BARABARANI
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya Tshs 3,043,200/=
Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ALHAMISI Tarehe 17/10/2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.


Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajw hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08/10/2019

114457502

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHAMED RAMADHAN**
anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.325/72** kilichotolewa na **LUGALO SEKONDARI IRINGA** mwaka 1987.


Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
USH/RB/398/09.

115457402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**John Y. Lori anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2335-0075 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Wazo Hill.**

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/KIJ/RB/360251/2019**

115457202

---

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GUARDIOLA: FODEN HAUZWI KWA BEI YOYOTE



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola asema kuwa, Phil Foden ndiye mchezaji pekee kwenye kikosi cha Manchester City ambaye hatauzwa.

Kinda huyo raia wa Uingereza ameamua kutuliza maisha yake kwenye klabu hiyo licha ya kwamba amekuwa hapati nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Guardiola anaamini kuwa Foden (19), ni silaha ya baadaye ya City, kwamba atakuwa 'mchawi' wao wakati David Silva atakapoachana na timu hiyo mwishoni mwa msimu.

Guardiola alisema: "Hatukumpa tu Foden mkataba mpya kwa bahati mbaya. Huyu ni mchezaji pekee ambaye hatuwezi kumuuza katika mazingira yoyote yale, ni yeye pekee. Hauzwi hata kwa Euro 500 milioni," alisema.

"Phil haendi kokote, Phil ni Man City. Hatuwezi kumsajili mtu mwingine yeyote kwenye nafasi hiyo. David Silva atakapoondoka, basi Phil atakuwa mchawi wetu."

City hawataki kufanya uzembe kama walivyofanya huko nyuma, walipomruhusu Jadon Sancho aende Borussia Dortmund na Brahim Diaz kwenda Real Madrid, ambapo huko wamekuwa kwenye viwango bora na msaada kwa timu zao.

# Van der Sar aisikitikia Man United

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, Edwin Van der Sar, ametoa kauli nzito kwa klabu yake ya zamani kutokana na mwenendo mbaya msimu huu.

Nguli huyo alisema wachezaji wa United wamepoteza mfumo wao hali inayochangia timu hiyo kuyumba.

Van der Sar anakumbuka namna Manchester United ilivyokuwa na nguvu enzi zao ikiwa chini ya akina Roy Keane, Gary Neville, Paul Scholes na Rio Ferdinand.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer yuko kikaangoni baada ya kupata matokeo mabaya msimu huu baada ya kuvuna pointi tisa na ipo nafasi ya 12 katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Kipigo cha bao 1-0 ilichopata kutoka kwa Newcastle United Jumapili kimemuibua nyota huyo aliyecheza kwa mafanikio Old Trafford.

"Nadhani wanapaswa kujitathimini, wakati ule mkiwa ndani ya vyumba vya kuvalia nguo utakutana na akina Ryan Giggs,"alisema nguli huyo aliyecheza United kwa muda wa miaka sita.



# Mourinho bado ana ndoto kufundisha England



**LONDON,** England

JOSE Mourinho amebainisha kwamba, ndoto zake ni kuinoa tena klabu ya Ligi Kuu England.

Mourinho ameitosa ofa aliyowekewa mezani na klabu ya Lyon ya Ufaransa huku akiwaambia wazi kwamba "nataka kazi England'.

Mourinho, kocha mtata wa zamani wa Chelsea na Manchester United amekuwa hana kazi tangu Desemba mwaka jana na mapema wiki hii alifuatwa na klabu ya Lyon ya Ufaransa kwa ajili ya kuchukua kazi ya kocha aliyefukuzwa, Sylvinho lakini amegoma.

Sylvinho, mlinzi wa zamani wa Arsenal na Barcelona amefukuzwa kazi katika klabu hiyo ya Ufaransa baada ya kuambulia pointi tisa katika mechi tisa akipoteza mechi nne na kushinda mechi tatu. Sylivinho ndio kwanza alikuwa ameajiriwa Mei mwaka huu.

Mabosi wa Lyon waliamua kwenda kasi kwa Mourinho wakiamini kwamba angekuwa mtu mwafaka wa kuwapeleka katika "Top Four", hata hivyo kocha huyo Mreno ambaye pia amewahi kufundisha Porto, Inter Milan na Real Madrid aliwafahamisha kwamba mpango wake ni kurudi tena katika mchakamchaka wa Ligi Kuu England.

Inadaiwa kwamba Mourinho amekuwa akikinyemelea kiti cha Mauricio Pochettino katika klabu ya Tottenham Hotspurs baada ya kocha huyo kuandamwa na matokeo mabaya katika siku za karibuni ambapo Spurs imejikuta nje ya ushindani wa ubingwa na "Top Four" mpaka sasa.

## HABARI MICHEZO

# Matic afikiria kuondoka United


**MANCHESTER,** England

KIUNGO mkongwe wa Manchester United, Nemanja Matic, hana furaha na benchi analopigwa na kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer na yupo tayari kutimka klabuni hapo katika dirisha la Januari huku Inter Milan wakidhamiria kumnasa.

Mkataba wa staa huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 31, unatarajiwa kumalizika mwisho mwa msimu huu, lakini Matic hataki kusubiri na badala yake anataka kuungana na kocha wake wa zamani katika klabu ya Chelsea, Antonio Conte.

Inter walimtaka Matic katika dirisha kubwa lililopita la majira ya joto, lakini United waligoma kumuuza. Hata hivyo, kocha Solskjaer anapendelea zaidi kuwapanga Paul Pogba na Scott McTominay huku Matic akisugua benchi.

Hali hiyo haimfurahishi Matic ambaye alizungumza wazi kwamba hajui kwanini anaachwa benchi na akabainisha kuwa kama timu hiyo itakuwa na matokeo mabaya kocha huyo anapaswa kuwajibika kwa sababu yeye ndiye anayeamua nani acheze na nani akae benchi.



# ZAHA: ARSENAL MVUMILIENI PEPE



**LONDON,** England

WILFRIED Zaha amewaambia mashabiki wa Arsenal kumvumilia na kumpa muda mshambuliaji wao mpya, Nicolas Pepe na sio kuanza kumsakama mapema baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 72 kutoka Lille.

Arsenal waliwasaka sana Zaha na Pepe kwenye dirisha lililopita la uhamisho wa majira ya kiangazi na matokeo yake waliishia kumnasa staa huyo kutoka Lille, ambapo wote ni wa kutoka taifa moja - Ivory Coast.

Baada ya kukwama kwenye bei ya Zaha, kocha Unai Emery alifungua pochi kwa kumnasa Pepe kwa mkwanja ulioweka rekodi ya uhamisho kwenye klabu yake hiyo ya Emirates.

Kutokana na kunaswa kwa fedha nyingi, mashabiki wengi wamekuwa wakitegemea mambo matamu kutoka kwa Pepe, jambo linalomfanya kuwa kwenye presha kubwa pindi anaposhindwa kufanya vitu vya kuwafurahisha.

Lakini, Zaha anaamini staa mwenzake huyo wa kimataifa wa Ivory Coast atatulia na kufanya mambo.

"Nimeona kwenye mitandao ya kijamii, nimeona kila kitu na ninachokiona anahitaji tu muda. Amekuja kutoka kwenye ligi tofauti na pia bado angali kijana mdogo," alisema Zaha.

"Kuna hili suala la bei yake, lakini hilo hakujipangia, watu ndio walimpangia, hivyo lisitazamwe na kiwango chake, mambo hayapo hivyo kabisa."

# Pioli kocha mpya AC Milan

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan ya Italia imemtangaza, Stefano Pioli kuwa kocha wake mpya akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Marco Giampaolo aliyetimuliwa klabuni hapo Jumanne, baada ya kuhudumu kwa muda wa miezi mitatu na nusu.

Pioli, raia wa Italia mwenye umri wa miaka 53, anakuwa kocha wa tisa, tangu AC Milan ilipotwaa ubingwa wa Serie A kwa mara ya mwisho mwaka 2011.

Kocha huyo ambaye amewahi kuvinoa vikosi vya klabu za Inter Milan, Fiorentina na Lazio anesemaini mkataba wa miaka miwili, kwa lengo la kuirejesha AC Milan kwenye ushindani wa kweli.

Mtaliano huyo atawajibika kurekebisha makosa yote ndani ya kikosi cha AC Milan, ili kufanikisha mipango itakayoiondoa klabu hiyo kwenye nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi ya Serie A, huku kukiwa na tofauti ya alama tatu dhidi ya timu zilizo kwenye ukanda wa kushuka daraja.


Mwishoni mwa juma lililopita AC Milan iliifunga Genoa mabao 2-1, huku mlinda mlango Pepe Reina akiokoa mkwaju wa penalti dakika za lala salama, na kuifanya klabu hiyo kupata ushindi watatu msimu huu, kati ya michezo saba waliyocheza.

Tayari AC Milan wamepoteza michezo mitatu dhidi ya wapinzani wao wa jadi Inter Milan, Torino na Fiorentina.

Meneja aliyetimuliwa klabuni hapo Giampaolo mwenye umri wa miaka 52, alitangazwa kuchukua nafasi ya Gennaro Gattuso mwezi Juni mwaka huu, baada ya mchezaji huyo wa zamani kujiuzulu, kufuatia kushindwa kufika malengo ya kuipeleka timu yake katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# DONDO KA
## MAGAZET YA




# MAN CITY VITANI KUMWANIA DIAS

●●● Beki huyo Mreno wa Benfica anawaniwa pia na Manchester United...

**MANCHESTER,** England

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City wametajwa nao kuanza mchakato wa kuwania saini ya beki wa kati wa Benfica, Ruben Dias, itakapofika kipindi cha usajili cha dirisha dogo la Januari.

**Kocha wa City, Pep Guardiola, ameamua kuingia katika vita ya kuwania saini ya beki huyo ili kuimarisha safu yake ya ulinzi.**

Uamuzi huo pia unatokana na beki wake, Aymeric Laporte, ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu kushindwa kuwapo kwenye kikosi cha kwanza tangu kuanza kwa kampeni ya kutetea taji la Ligi Kuu England ambalo wanalishikilia.

Katika vita hiyo, City inajiandaa kuchuana na mahasimu wao, Manchester United kumwania mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno ambaye anatajwa kuwa na thamani kubwa, limeandika gazeti la The Mirror.

Mkataba wa Dias na Benfica unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2024 na klabu yake inatarajia kuboresha mkataba wa Mreno huyo na kufikia thamani ya pauni milioni 79 kwa klabu itakayokuwa tayari kumnunua. City imeshindwa kuendelea kujiimarisha kwenye idara yake ya ulinzi katika kipindi cha majira ya joto, tangu alipoondoka aliyekuwa nahodha wa timu hiyo, Vincent Kompany.

Laporte ambaye alikuwa majeruhi wa goti kwa muda mrefu, anatarajiwa kurejewa mapema mwakani, wakati John Stones naye pia hayuko kikosini kutokana na kutokuwa fiti.

Gazeti la The Sun, liliandika mapema wiki hii kuwa, United wameweka wazi nia ya kumsajili beki huyo mwenye umri wa miaka 22.

Taarifa zaidi zilisema kuwa, United ilianza kufanya mchakato wa kumhamisha Mreno huyo katika kipindi cha majira ya joto lakini walishindwa kukamilisha mipango yao na sasa wanarejea tena kuwania huduma ya mchezaji huyo.

Dias ameichezea Benfisa mechi 85 katika misimu miwili aliyoitumikia akitokea katika kikosi cha vijana cha timu hiyo, na ameshinda mechi 13 akiwa na Timu ya Taifa ya Ureno ambayo alianza kuichezea mwaka jana.

## ZISIKUPITE

### EVERTON YAMTEGA SILVA

KOCHA wa Everton, Marco Silva, amepewa mechi tatu ili kuangalia hatima ya kibarua chake baada ya kuwa na mwanzo mbaya msimu huu. Klabu hiyo ya Goodison Park iko katika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa Ligi Kuu England ikiwa na pointi saba baada ya kushuka dimbani mara nane. ***(Star)***

### LEICESTER KUIKAMUA UNITED

MABOSI wa Manchester United wanajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 130 ili kumsajili kiungo wa Leicester City, James Maddison na beki Ben Chilwell, ambao kila mmoja ana umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### CHILWELL ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa kushoto wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell (22), mara baada ya adhabu yao ya kufungiwa kusajili itakapomalizika. ***(Mail)***

### UNITED KUSAJILI NANE

MANCHESTER United imesema kuwa inataraka kusajili wachezaji wapya nane katika vipindi viwili vinavyokuja vya majira ya joto na tayari imeshaorodhesha nyota hao inaowahitaji ili kuimarisha kikosi chake. ***(Telegraph)***

### MANDZUKIC, CAN KUTOLEWA

JUVENTUS iko tayari kumtoa straika wa Croatia, Mario Mandzukic (33) na kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Emre Can (25) ili kubadilishana na Manchester United kwa lengo la kumnasa kiungo wao Mfaransa Paul Pogba (26). ***(Sun)***

### SPURS KUMUUZA ERIKSEN

TOTTENHAM Hotspur inaamini itafanikiwa mpango wake wa kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27) katika kipindi cha dirisha dogo la Januari ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata fedha badala ya kumwona akiondoka kama mchezaji huru ifikapo majira ya joto. ***(Mirror)***

### PALMIERI ATAJWA JUVENTUS

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, ameweka wazi malengo yake ya kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Italia, Emerson Palmieri (25), kutoka katika klabu yake ya zamani aliyowahi kuifundisha ya Chelsea. ***(Express)***

### ARSENAL YAMTAKA KOKCU

ARSENAL imeanza mchakato wa kutafuta saini ya kiungo wa Feyenoord, Orkun Kokcu, ambaye ana umri wa miaka 18 na thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 20. ***(Mail)***

### KOULIBALY AIBURUGA UNITED

MANCHESTER United inaendelea na mipango ya kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Kalidou Koulibaly, mwenye umri wa miaka 28 ambaye sasa anaichezea Napoli. ***(Express)***

### PIQUE AINGIA SOKONI

BEKI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Gerard Pique (32), amekaribia kukamilisha mchakato wa kuinunua klabu inayoshiriki Ligi ya Taifa England iitwayo, Notts County katika kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

## HABARI MICHEZO




Washindi wa promosheni ya Faidika na Jero inayoendeshwa na Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya SportPesa wakiwa na zawadi zao za simu kwenye ofisi za SportPesa. Kutoka kushoto ni Omary Muchande, Shabani Nchi na Yassini Ahmed. **PICHA: SPORTPESA**

# *Watatu washinda simu za SportPesa*

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wa promosheni ya Faidika na Jero inayoendeshwa na Kampuni ya mtandao wa Tigo kwa kushirikiana na SportPesa wameendelea kufurahia huduma mbalimbali huku wakipata nafasi ya kujishindia simu, imefahamika.

Zawadi kubwa katika promosheni hiyo inayotarajiwa kufanyika mwishoni wa mwezi huu ni gari aina ya Renault Kwid.

Wiki iliyopita SportPesa ilitangaza washindi saba kutoka mikoa mbalimbali ambapo washindi watatu wakitokea Dar es Salaam na wikii hii SportPesa imetangaza washindi wengine saba wanne wakitokea hapa jijini.

Washindi wa wiki hii kutoka hapa jijini ni Farid Ally kutoka Temeke, Ibrahim Mudi Kubamba wa Ilala, Mfaume Kungulilo kutoka Mbezi na Mecklord Kamnde wa Tabata Segerea wakati Said Navake anatoka Mtwara, Salumu Gustafu (Morogoro) na Erick Kiwala ni kutoka mkoani Iringa.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, alisema kuwa wanafuraha kuona wanaendelea kupata washindi kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini.

"Wiki hii ni wiki ya huduma kwa wateja hivyo basi sisi kama SportPesa tunapenda kuwajulisha wateja wetu kwamba tunawajali na kuwathamini maana sisi kwetu mteja ni mfalme. Huduma zetu ni saa 24 siku saba za wiki, tutahakikisha wahudumu wetu zaidi ya 100 wanasikiliza matatizo na mahitaji ya wateja.

# Kigwangalla mgeni Rock City Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hamisi Kigwangalla anatarajiwa kuwa mgeni ramsi katika mashindano ya mbio za Rock City Marathon zitakazofanyika Oktoba 20, mwaka huu jijini Mwanza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mbio hizo, Clement Mshana, alisema jana kuwa Waziri Kigwangalla ataungana na viongozi wengine waandamizi wa serikali kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella kushiriki katika mbio za kilomita 42.

"Uwepo wa Waziri mwenye dhamana na masuala ya utalii kwenye mbio hizi unatokana na yeye kuunga mkono agenda iliyobebwa na mbio hizi ambayo mbali na kukuza vipaji vya mchezo huo ni kutangaza utalii hususani katika ukanda wa Ziwa kupitia mchezo wa riadha," alisema Mshana.

Alisema kuwa maandalizi ya mbio hizo yako katika hatua za mwisho na jumla ya Sh. milioni 30 na medali, zimeandaliwa kwa ajili ya kutoa zawadi kwa washindi.

"Pamoja na kupata medali, washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 42 kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni nne kila mmoja wakati washindi wa pili wataondoka na Sh. milioni mbili na washindi wa tatu watapata Sh. milioni moja," alisema mratibu huyo.

Alisema kutakuwa pia na mbio za kilomita tano ambazo zitahusisha washiriki kutoka mashirika na taasisi mbalimbali na mbio hizo, zitaongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dkt. Philis Nyimbi huku pia washiriki wengine wakitarajiwa kuwa ni watu wenye ulemavu wa ngozi.

Aliongeza kuwa usajili wa mbio hizo umeshaanza kupitia vituo na mawakala walioko mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, Pwani na Arusha.




Wadhamini wa mashindano ya soka ya watoto wa umri chini ya miaka 13 wakionyesha makombe yatakayoshindaniwa katika michuano itakayofanyika Novemba 2, mwaka huu jijini Dar es Salaam. Kutoka kushoto ni Meneja wa Kampuni ya Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, George Nyanda, Meneja wa Matukio wa Kampuni ya Toyota Tanzania, Nadah Dhiyebi (katikati) na Mkurugenzi wa Mipango wa Selcom, Benjamini Mpango. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS DIMBANI DES.14

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Simba Queens inatarajia kukutana na watani zao Yanga Princess katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania utakaochezwa Desemba 14 mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

**Mchezo huo utakuwa ni wa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo inayotarajiwa kushirikisha klabu 12 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.**

Simba Queens inayofundishwa na Mussa Hassan "Mgosi" itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuwafunga watani zao katika mechi zote mbili za msimu uliopita.

Kwa sasa kikosi cha Yanga Princess kinanolewa na Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Edna Lema. Akizungumza jana jijini, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto alisema kuwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake 2019/20 utaanza Oktoba 26 mwaka huu kwa timu zote 12 kushuka uwanjani kuwania pointi tatu muhimu.

Kizuguto alisema kuwa katika raundi ya kwanza, mabingwa watetezi JKT Queens watakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Jamhuri kuwavaa Baobab Queens wakati Simba Queens itawakaribisha wageni kwenye ligi hiyo, Ruvuma Queens kutoka Songea.

Alisema kuwa Alliance Queens watawakaribisha Kigoma Sisterz kwenye Uwanja wa Nyamagana wakati TSC wao watachuana na Marsh Girls na Mlandizi Queens watavaana na Panama Girls kutoka mkoani Iringa huku Tanzanites Queens itacheza dhidi ya Yanga Princess kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kiongozi huyo alisema kuwa ligi hiyo itasimama kwa muda kuanzia Novemba 16 hadi 28 mwaka huu, kwa ajili ya kupisha mashindano ya Kombe la Chalenji kwa wanawake ambayo mwaka huu yanafanyika hapa nchini.

Alisema pia mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo unatarajiwa kumalizika Januari 30 mwakani.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 12, 2019
Nipashe



Man City vitani kumwania Dias UKURASA 30



Nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), na mshambuliaji wa KRC Genk ya Ubelgiji, Mbwana Samatta (kulia) akiwa na mke wake, Naima Mgange, baada ya wawili hao kufunga ndoa juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Bandari kupimana

**Na Mwandishi Wetu**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wanatarajia kuwakaribisha Bandari kutoka Kenya, katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Simba inatarajia kutumia mchezo huo ili kujiandaa na mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC, itakayochezwa Oktoba 23 kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema jana kuwa maandalizi ya mchezo huo, yamekamilika na wanatarajia kuutumia kujiimarisha kabla ya kukutana na Azam FC ambayo, nayo imetolewa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Rweyemamu alisema kuwa, katika mchezo huo, wanatarajia kuwatumia wachezaji wake sita kutoka kwenye timu ya vijana (Simba B) ili kuziba nafasi ya nyota wake nane walioko katika Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa na mchezo wake dhidi ya Rwanda.

Kikosi cha Bandari kinachonolewa na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Ben Mwalala, kilitarajiwa kuwasili nchini jana jioni tayari kwa mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

## Stars kamili yawasili Kigali

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kiliwasili salama jijini Kigali, Rwanda jana asubuhi, tayari kuwakabili wenyeji katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa utakaochezwa Jumatatu nchini humo.

Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Suleiman Matola, alisema jana kuwa uamuzi wa kwenda mapema Kigali, umetokana na kuhitaji nafasi zaidi ya kukiimarisha kikosi hicho katika eneo tulivu zaidi.

"Tumeshafika Rwanda, tuliamua kuja huku (Kigali) mapema kwa sababu zetu za kiufundi, kuna programu ambazo mwalimu alitaka tuzifanye tukiwa nje ya nyumbani, pia itawapa nafasi wachezaji kupumzika vema na kusubiri mchezo," alisema Matola.

Stars inatarajia kutumia mchezo huo wa kirafiki kama sehemu ya maandalizi ya kuwavaa Sudan katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) itakayochezwa Oktoba 18 mwaka huu mjini Omdurman.

# Yanga yakutana kuijadili Pyramids

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Lengo ni kupanga mikakati ya kuwamaliza Waarabu hapa nyumbani...

UONGOZI wa Yanga unatarajia kufanya kikao maalumu leo kwa ajili ya kupanga mikakati ya kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wao wa hatua ya mtoano wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids kutoka Misri, imeelezwa.

**Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema kuwa wameamua kuitisha kikao hicho, ili kugawa majukumu ambayo yataifanya timu yao ifanye vizuri katika mchezo huo wa kwanza na wa marudiano utakaochezwa baada ya wiki moja.**

Mwakalebela alisema kuwa wanaamini kikao hicho, kitatoa mwelekeo wa timu yao katika mashindano hayo ya kimataifa kwa kujipanga kurekebisha makosa yaliyobainika wakati walipokuwa wanashiriki kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tutakuwa na kikao kesho (leo), naamini mikakati na mipango ya kuhakikisha Waarabu "wanakufa" hapa hapa nyumbani inatimia, kuna vitu tumeshajifunza, mbinu mbalimbali tumezibaini wakati tunashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatutaki yajirudie huku tulikohamia," alisema Mwakalebela.

Kiongozi huyo aliongeza kwamba wanaamini nafasi ya kusonga mbele katika mashindano hayo wanayo na kinachotakiwa kufuatwa ni kujipanga imara.

"Tunataka kuhakikisha tunacheza vizuri hesabu zetu, hakuna kisichowezekana, tutajipanga na kukiandaa vema kikosi chetu kupata ushindi na kumaliza mchezo katika dakika 90 za nyumbani, tukienda Misri inakuwa ni kukamilisha ratiba," Mwakalebela alisema.

Katika kukiongezea makali kikosi chao, Yanga inatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki ikiwamo dhidi ya Pan African.

"Hatubabaishwi na hatutishwi na uwezo wao wa kifedha, tunasema Yanga bado tupo kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho, kwa bahati mbaya mpira unachezwa uwanjani, hauchezwi kwenye maneno, mechi tutahakikisha inamalizika Dar es Salaam," alisema Antonio Nugaz, Ofisa Mhamasishaji wa klabu hiyo.

Kabla ya kuwakaribisha Pyramids, Yanga itasafiri kwenda Mwanza kuwafuata Alliance FC na Mbao FC kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002